# Jarida la BUNGE

ISSN-085-6046 TOLEO LA NANE NOVEMBA, 2024




# Kishindo cha Dkt. Tulia IPU



Katibu Mpya akikabidhiwa Ofisi



Mkutano wa 53 wa CPA Kanda ya Afrika



Mashindano ya 38 ya SHIMIWI

# DIBAJI



**Ndugu Msomaji,**

Nakukaribisha kwenye Jarida la Bunge Toleo la Nane ambalo limeangazia kuhusu shughuli za Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge na makala nyingine elimishi kuhusu mambo mbalimbali ya Kibunge.

Kuhusu Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, toleo hili pamoja na mambo mengine limechambua Miswada iliyopitishwa na Bunge wakati wa Mkutano huo, taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa na Spika wa Bunge kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya Mwekezaji kwenye shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka Shamba hilo lililopo katika Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na hotuba ya Waziri Mkuu wakati akiahirisha Mkutano huo.

Aidha, kwa upande wa Mikutano ya Vyama vya Kibunge vya Kimataifa, toleo hili limebeba habari kuhusu Mkutano Mkuu wa 53 wa CPA Kanda ya Afrika, uliofanyika Jijini Arusha pamoja na habari kuhusu Mkutano Mkuu wa 149 wa IPU uliofanyika Jijini Geneva, Uswisi.

Pia toleo hili lina makala ambazo zinaendelea kuchambua kwa kina kuhusu Usimamizi wa Kibunge wa matumizi ya fedha za umma, Misingi ya Utaratibu na Uendeshaji wa Vikao vya Bunge pamoja na Umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa Majukumu na Madaraka ya Bunge.

Kwa upande wa Historia kuhusu Bunge la Tanzania, toleo hili lina makala kuhusu Spika wa Kwanza Mzalendo na pia kuhusu Spika wa kwanza mzawa.

Pamoja na hayo masuala mengine ambayo yameandikwa katika toleo hili ni ziara ya Spika wa Bunge la Comoro katika Bunge la Tanzania, NMB Bunge Bonanza na ushiriki wa Watumishi wa Bunge katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI).

Nawatakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

**Ndugu Baraka I. Leonard**
**Katibu wa Bunge.**


**BODI YA UHARIRI**

**Mlezi wa Jarida**

**Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb)**
**Spika wa Bunge**

**Bodi ya Uhariri**

**Mwenyekiti**
**Ndg. Baraka Leonard**

**Makamu Mwenyekiti**
**Ndg. Zuhura Mtatifikolo**

**WAJUMBE**
**Ndg. Athuman Hussein, *ndc***
**Ndg. Hanifa Masaninga**
**Ndg. Abdallah Hancha**
**Ndg. Chacha Nyakega**

**WAHARIRI**

**Ndg. Lawrence Raphaely**
**Mhariri**

**Ndg. Debora Sanja**
**Mhariri Msaidizi**

**Msanifu**
**Ndg. Edwin K. Tongora**



**Limeandaliwa na:**
**Ofisi ya Bunge**
**Mtaa wa Makole**
**S.L.P 941,**
**41105 DODOMA.**
Nukushi: +255 26234218
**Simu: +255 26 232276-5**
**Barua Pepe: cna@bunge.go.tz**

# YALIYOMO


Kishindo cha Dkt. Tulia katika Mkutano wa 149 wa IPU..................1

Katibu wa Bunge: Endeleeni Kufanya Kazi kwa Kujituma................4

Waziri Mkuu: Andaeni Mazao yanayokomaa Haraka.......................7

Dkt. Mpango: Mabunge himizeni Uwekezaji katika Kilimo................9

Bunge: Serikali Badilisheni Umiliki Shamba la Malonje.................12

Bunge lapitisha Miswada 8 katika Mkutano wa 16........................14

Dkt. Salema Achaguliwa Mbunge EALA...................................16

Misingi ya Utaratibu na Uendeshaji wa Bunge............................17

Mfahamu Spika wa Kwanza Mzalendo....................................21

Usimamizi wa Kibunge wa Matumizi ya Fedha za Umma...............23

Spika wa Comoro atembelea Bunge la Tanzania.........................26

Kamati: Sheria zilinde maslahi ya nchi...................................28

Dkt. Ndugulile achaguliwa WHO..........................................29

Kutoka Chifu hadi Spika wa Bunge.......................................30

Umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa majukumu .....33

NMB Bunge Bonanza lahamasisha kushiriki katika Uchaguzi............37

Watumishi wa Bunge katika mashindano ya 38 ya SHIMIWI.............38














# Kishindo cha Dkt. Tulia Ackson ka




*Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson akizungumza wakati wa Mkutano Mkuu wa 149 wa IPU uliofanyika Jijini Geneva, Uswisi.*

*Na. Omary Machunda*

Wakati historia ikiendelea kuandikwa kwenye kumbukumbu za Umoja wa Mabunge Duniani kuongozwa kwa mara ya kwanza na Spika mwanamke kutoka nchi ya ulimwengu wa tatu, nao watanzania wameendelea kutembea kifua mbele baada ya nchi yao iliyounganishwa kwa udongo wa Tanganyika na Zanzibar, kumtoa kiongozi huyo.

Ni takriban mwaka mmoja sasa tangu Dkt. Tulia Ackson alipochaguliwakuwaRaiswa31wa IPU kwenye Mkutano uliofanyika mnamo tarehe 27 Oktoba, 2023, Jijini Luanda, Angola na kuanza kuitumikia nafasi hiyo kwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa katika Katiba ya IPU.

Dkt. Tulia alianza kwa kutembelea mataifa mbalimbali miongoni mwa nchi wanachama wa umoja huo kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali zinazozikabili nchi wanachama wa IPU na hatimaye kuifanya dunia kuwa mahali salama pa kuishi wanadamu.

Alianza kwa kuripoti kazini yalipo Makao Makuu ya IPU Jijini Geneva, Uswisi na kupokelewa na watumishi wa Ofisi hiyo tayari kuanza kutekeleza majukumu yake. Aidha, katika ziara ya kwanza nje ya Ofisi ya Geneva, Dkt. Tulia alitembelea nchi ya Israeli kisha Palestina na baadaye mataifa mbalimbali yakiwemo China, Misri, Austria, Marekani na India ikiwa ni baadhi tu ya mataifa aliyotembelea.

Hatimaye alirudi katika ardhi ya Jiji la Geneva mahali pa utalii na Jiji la amani linalohodhi mikutano mingi ya kimataifa katika viunga vyake.

Katika Mkutano Mkuu wa 149 wa IPU uliofanyika kuanzia tarehe 13 Oktoba hadi 17 Oktoba 2024 Rais wa IPU Dkt. Tulia alifungua makucha yake na kuonesha uimara, ushupavu na misimamo isiyotetereka akisisitiza heshima

# tika uwanja wa siasa za Kimataifa

miongoni mwa wajumbe pamoja na kuheshimu kanuni na sheria zinazoongoza IPU.

Ilikuwa siku ya Jumatatu tarehe 14 Oktoba 2024 wakati akiendesha kikao cha Kamati ya Amani na Usalama wa Kimataifa (Standing Committee on Peace and International Security) kilichokuwa kikiangazia jukumu la Wabunge na Mabunge katika kuzuia migogoro mbalimbali ili isigharimu raslimali za umma katika kutatua migogoro hiyo.

Dkt. Tulia alitoa nafasi kwa wajumbe wa Mkutano huo kuuliza maswali pamoja na kutoa mawazo yao juu ya hoja iliyopo mezani kuhusu mustakabali wa amani duniani hasa kwa kuyamulika mataifa yenye migogoro ya ndani na mataifa yanayopigana sehemu mbalimbali duniani.

Katika kikao hicho baadhi ya Wajumbe walihoji uhalali wa yeye kufanya ziara nchini Urusi na kukutana na Rais wa nchi hiyo Mheshimiwa Vladmir Putin.

Hali kadhalika, wapo wajumbe waliohoji kwanini Dkt. Tulia hakukutana kwanza na Rais wa Ukraine Mheshimiwa Volodymyr Zelenskyy yamkini ilikuwa ni muhimu zaidi kwa wakati huo kuliko kukutana na Rais Putin, kwa mtazamo wa wajumbe hao.

Mfano, mjumbe kutoka Lithuania aliuliza, "Mheshimiwa Rais unajisikiaje kushikana mikono na mhalifu wa kivita Vladmir Putin kutoka katika utawala wa kigaidi wa Urusi na nani hasa alikupa mamlaka ya kuiwakilisha IPU katika hilo na ni faida zipi zilizopatikana katika ziara hiyo kwenye maendeleo ya demokrasia kama sio kunufaisha propaganda za nchi ya Urusi? Na je, unakubali kuwa kuanza ziara nchini Urusi kabla ya kwenda Ukraine lilikuwa kosa kubwa sana na unalijutia?"

Haikuishia hapo, mjumbe kutoka nchini Ukraine alizungumzia hali ilivyo nchini humo kutokana na vita vinavyoendelea baina ya nchi hiyo na Urusi na kutaka kujua kama Rais huyo wa IPU anatambua hali hiyo na endapo kuna hatua zozote alizochukua kushughulikia mgogoro huo.

Alisema, "ulituambia kuwa ulikutana na Rais Putin, nataka wote tutambue kuwa ziara yako ilifanyika siku chache tu baada ya makombora kutoka Urusi kuangamiza hospitali ya watoto kule Ukraine, swali langu la kwanza ni lini Wajumbe wa IPU watapata taarifa za kikao chako na Rais Putin, swali la pili, je, ulijadiliana na Putin juu ya Maazimio ya IPU yanayokemea uvamizi wa Urusi nchini Ukraine? Na swali la tatu, je, mlijadili juu ya majeshi ya Urusi kuteka watoto wa Ukraine?"

Aidha, mjumbe kutoka nchini Iraq alimlaumu Rais wa IPU kwa kutembelea Urusi na Israeli badala yake akamtaka kutembelea Ukanda wa Gaza pamoja na Kusini mwa Lebanon ili kupata picha halisi ya hali ilivyo katika maeneo hayo na kutafuta ufumbuzi.

Akijibu maswali hayo, Dkt. Tulia alianza kwa kuwataka wajumbe hao kuheshimiana na kumheshimu yeye kama kiongozi mkuu wa taasisi hiyo kwa kuwa walimchagua kwa hiari yao na kumpa majukumu ya kutekeleza kwa mujibu wa kanuni na sheria zinazosimamia umoja huo.

Alisema, "Waheshimiwa Wajumbe, kuna swali limeulizwa na mjumbe kutoka Iraq akirejea taarifa niliyoiwasilisha kwenu na ameuliza kwa nini nilitembelea Urusi na sio Gaza, nataka kuwajulisha wajumbe wenzangu kuwa mnapaswa kujua kuwa Novemba mwaka jana nilitembelea Palestina na Israeli na nilikutana na viongozi wa huko na hiyo ilikuwa ziara yangu ya kwanza baada ya kuwa kiongozi wa IPU, hivyo sio kama nadharau kile kinachoendelea Mashariki ya Kati, Lebanon, Gaza na kilichotokea kule Israeli."

Aliongeza kuwa, "ninaichukulia kwa uzito unaolingana migororo yote inayoendelea na pia nataka nanyi muelewe kuwa migogoro tunayoizungumzia kuhusu Mashariki ya Kati pamoja na Ukraine sio migogoro pekee ambayo IPU inaitazama, tunatazama yanayoendelea Yemen, Syria, Sudan, Afrika Magharibi na Kongo DRC."

Akiendelea kujibu maswali hayo, Dkt. Tulia aliongeza kwa kusema, "Lithuania imeuliza maswali maalum kwamba nani alinipa mamlaka ya kutembelea Urusi na kwanini haikuwa Ukraine kwanza? Barua zilitumwa kwa nchi zote mbili na kama mtahitaji nakala mnaweza kupata maana sio za siri."

Aliongeza kuwa, "ziara yangu ilikuwa nianzie Ukraine, lakini Ukraine walijibu kuwa siku tunayopaswa kutembelea huko Rais Zelenskyy na Spika wa Bunge watakuwa New York kushiriki Mkutano wa NATO, je ningeweza kuwazuia wasiende huko? Hapana, sina mamlaka hayo, hivyo, je, ningeacha kwenda Urusi kwa kuwa Ukraine imeshindwa kunipokea kwa sababu ya kukosa muda kutokana na mkutano wao wa NATO?

Pia, Dkt. Tulia aliwashangaa wajumbe wanaotilia shaka mamlaka yake ya kufanya ziara katika nchi hizo huku akitanabaisha kuwa ana uhakika wajumbe hao wasingeonesha

hali hiyo endapo angefanya ziara katika nchi wanazotaka wao.

Alisema, “IPU inasimamia mijadala na diplomasia ya kibunge na kwa sababu hiyo nilifanya kile nilichokifanya na ninadhani kuwa ningeweza kupewa pongezi angalau kwa juhudi zote nilizozifanya na sio kuhukumiwa kwa mambo ambayo sikuyafanya.”

Aliendelea kwa kuwauliza wajumbe hao kwa nini hawajauliza maswali hayo juu ziara yake ya Israeli na Palestina na endapo wangemuuliza maswali ya namna hiyo kama angefanya ziara nchini Sudan na sehemu nyingine bali wamemuuliza maswali hayo kwa kuwa amefanya ziara nchini Urusi jambo ambalo kwa mtazamo wake anaona haliko sawa.

Aliendelea kuongeza kuwa, “naomba muwe na imani, mlinichagua niwe Rais ili nitumikie kwa mujibu wa mamlaka hayo na nadhani hamnitendei haki, maswali mliyoniuliza nimeyajibu kwa uhakika na kwa uwezo wangu wote na ninyi mnajua kuwa nisingeweza kukutana na Rais Putin kama sio juu ya jenda ya mgogoro wake na Ukraine.”

Alihimiza kuwa, “mimi sio Mungu, mimi sio malaika, mimi ni binadamu nafanya ninachoweza kufanya kilicho ndani ya uwezo wangu na ninaomba mniheshimu kama ninavyowaheshimu na naomba mnipe nafasi niongoze chombo hiki kulingana na taratibu zilizowekwa.”

Dkt. Tulia alimalizia kwa kuwakumbusha kuwa inawezekana miongoni mwa wajumbe wa IPU wamo wanaodhani kwamba bado waafrika wanaendelea kutaliwa kifikra na mataifa ya Magharibi kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni, jambo ambalo kwa sasa ni historia.

## Aungwa mkono kwa msimamo wake

Mijadala imeendelea kusikika maeneo mbalimbali nchini hususan kupitia majukwaa kama vyombo vya habari na kurasa za mitandao ya kijamii kama vile Youtube, Instagram na Jamii Forums ambapo Watanzania wa kada tofauti wamempongeza Dkt. Tulia kwa kutoficha misimamo yake wakati wa kuiongoza IPU.

Mathalani, wachambuzi Ally Masubi, Henry Mwinuka na Fredrick Bundala kupitia ukurasa maarufu wa SnS (Simulizi na Sauti) unaoendesha mijadala yake katika mtandao wa Youtube na Instagram walilichambua kwa upana jambo hilo katika makala yao ya tarehe 9 Oktoba 2024.

Aidha, tarehe 15 Oktoba 2024 Jukwaa la Mabunge ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC-PF) walitoa taarifa kutoka Jukwaa hilo yenye kuashiria mshikamano na kumuunga mkono Rais wa IPU pamoja na kumtia moyo huku wakimtaka aendelee kuliongoza Jukwaa hilo pasipo kutetereka na sehemu ya taarifa hiyo ikimkumbusha kuwa nchi za SADC ziko nyuma yake.

“Tunaamini kwamba Dkt. Tulia Ackson amefanya kazi yake ipasavyo kwa kutumia mamlaka yake kukutana na Rais wa Urusi na hata vyombo vya habari vya Kimataifa viliripoti kuwa kikao hicho kililenga kujadili namna ya kuimarisha amani duniani na hili limefanyika chini ya mwamvuli wa IPU inayoongozwa na Dkt. Tulia Ackson,” ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Dkt. Tulia Ackson anaendelea kutumikia cheo hicho cha Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) hadi Oktoba 2026 pasipo kuweka kando majukumu yake kama Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafasi atakayoitumikia kwa sasa.



# Katibu wa Bunge: Endeleeni kufanya Kazi kwa kujituma



*Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard.*

*Na: Deonisius I. Simba*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uteuzi huo wa Ndg. Leonard ulitangazwa Septemba 16, 2024 na baadaye akaapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Septemba 19, 2024, Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Ndg. Leonard ambaye anakuwa Katibu wa Bunge wa 13 anachukua nafasi ya Ndg. Nenelwa Mwihambi ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Akizungumza katika kikao kilichowakutanisha Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa Oktoba 26, 2024, Ndg. Leonard aliwataka Watumishi wa Ofisi ya Bunge kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kwa kujituma huku wakizingatia kanuni na sheria za kazi.

"Nimeelezwa kwamba mnafanya kazi kwa kujituma na mimi nimeshuhudia hilo. Hongereni kwa hilo na naomba muendelee na ari hiyo ya kufanya kazi kwa kujituma," alisema.

Katibu wa Bunge aliwaeleza pia Watumishi hao matarajio yake kwao kwamba anatarajia waendelee kufanya kazi kwa ushirikiano, nidhamu, upendo na weledi wa hali ya juu.

"Kikao hiki ni muhimu kwangu ili niweze kuwaeleza yale ninayotarajia kutoka kwenu na pia niwaeleze ahadi zangu kwenu," alisema.

Katibu wa Bunge aliwakumbusha Watumishi kwamba ushirikiano hauwezi kuwepo sehemu yenye majungu na fitina.

"Naamini katika kufanya kazi kwa ushirikiano. Nafananisha utendaji kazi na timu kama ya mpira. Ushirikiano ndio



*Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Ildephonce Leonard akiongoza kikao cha Menejimenti ya Ofisi ya Bunge.*

hatimaye unaoleta ushindi na watu wanashangilia. Ushirikiano hauwezi kujengwa sehemu yenye majungu. Taasisi yenye amani na upendo kazi inaenda vizuri," alisema.

Katibu wa Bunge pia aliwaeleza Watumishi hao kwamba hatowaendekeza wala hatowavumilia wale wote watakaokuwa wanafanya kazi kwa fitina, majungu, upendeleo na



*Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Leonard akisalimiana na Watumishi wa Ofisi ya Bunge waliojitokeza kumpokea wakati anawasili kwa mara ya kwanza Ofisini Jijini Dodoma.*

kwa kusababisha migawanyiko.

"Mfanye kazi kwa upendo na palipo na upendo hakuna fitina wala majungu. Sitoweza kuelewana na mtu anayependelea na anayegawanya watu," alisema.

Mbali na hayo Katibu wa Bunge aliwaeleza Watumishi hao kwamba yeye ni mtu anayefikika na siku zote milango yake itakuwa wazi kwa ajili ya kuzungumza na Watumishi au Mtumishi yeyote pale kutakapokuwa na changamoto yoyote ya kazi.

"Mimi nafikika kwa hiyo kama kuna tatizo nitafute kwenye simu au njoo Ofisini tuzungumze," alisema.

Sambamba na matarajio hayo Katibu wa Bunge amewaeleza Watumishi hao kwamba iwapo watafanya kazi kulingana matarajio yake ahadi yake kwao ni kutengeza mazingira wezeshi ya kufanya kazi.

"Haya ninayotarajia kutoka kwenu kama mtayazingatia ahadi yangu kwenu ni kujenga mazingira wezeshi ya kufanya kazi," alisema.

Kwa upande mwingine, aliyekuwa Katibu wa kwanza wa Bunge Mwanamke, Bi. Nenelwa Mwihambi, amebadilishiwa majukumu hayo baada ya kutumikia nafasi hiyo kwa miaka 3 na miezi 4.

Bi. Nenelwa aliteuliwa kuwa Katibu wa Bunge Mei 15, 2021 akichukua nafasi ya aliyekuwa Katibu, Ndg. Stephen Kagaigai ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC).

Kabla ya uteuzi huo, Bi. Nenelwa alikuwa Mkurugenzi wa idara ya Shughuli za Bunge chini ya Katibu wa Bunge, Ndg. Kagaigai.



*Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard katika picha ya pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Bunge mara baada ya kuzungumza nao katika ukumbi wa Pius Msekwa Jijini Dodoma.*





*Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Leonard katika picha ya pamoja na aliyekuwa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc, wakati wa makabidhiano ya Ofisi Jijini Dodoma.*

# Waziri Mkuu: Pandeni Mazao yanayokomaa Haraka

Na. Lawrence Raphaely

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa amewaasa wananchi kupanda aina ya mazao mbalimbali yanayokomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili ukame kufuatia utabiri wa hali ya hewa kuonesha kwamba mvua zitakuwa chini ya wastani.

Waziri Mkuu aliyasema hayo wakati akitoa hotuba ya kuhitimisha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliomaliza tarehe 6 Septemba, 2024 Jijini Dodoma.

"Utabiri unaonesha kuwa mvua zitakuwa chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengine yanayopata mvua hizo na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha," alisema.

Aliongeza kuwa utabiri huo unaashiria kuwa shughuli za uzalishaji wa mazao ya chakula zitaathirika hali inayoweza kupunguza utengamano wa upatikanaji wa chakula katika maeneo yanayopata mvua hizo na maeneo mengine ya nchi.

"Kutokana na mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu ni vyema tukachukua tahadhari mapema ili tuhakikishe tunazalisha mazao yanayokomaa kwa muda mfupi na kuwa na uhakika wa utoshelevu wa chakula," alisema.

Alisema pia kwa hapa nchini mvua za vuli ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua ambayo yanajumuisha Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro.

Waziri Mkuu pia alisema katika msimu huu wa kilimo wa mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kama ilivyofanyika katika misimu iliyotangulia.

Alisema Serikali itatoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi kwa wakulima kwa kutambua mwenendo wa uzalishaji wa zao la mahindi na ongezeko la mahitaji yake ndani na nje ya nchi katika msimu wa 2024/2025.

"Kipekee nitumie nafasi hii



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa akitoa hotuba ya kuhitimisha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliomaliza tarehe 6 Septemba, 2024 Jijini Dodoma



*Waheshimiwa Wabunge wakimpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa mara baada ya kutoa hotuba ya kuhitimisha Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliomaliza tarehe 6 Septemba, 2024 Jijini Dodoma*

kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuendelea kutoa pembejeo muhimu kwa wakulima na hivyo kuchagiza maendeleo ya sekta ya kilimo kwa ajili ya manufaa ya wakulima na Taifa kwa ujumla" alisema.

Alisema uzalishaji wa ndani wa mbolea na mbegu bora unaendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ambapo uzalishaji wa mbolea sasa umeongezeka kutoka tani 84,696 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 158,628 msimu wa 2023/2024.

Aidha alisema uzalishaji wa ndani wa mbegu zilizothibitishwa ubora umeongezeka kutoka tani 42,096 kwa msimu wa 2022/2023 hadi kufikia tani 56,114 msimu wa 2023/2024.

"Hali hii inaonesha kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa pembejeo ikiwa ni hatua mahususi ya kuchangia utoshelevu wa pembejeo za kilimo ndani ya nchi," alisema.

Kuhusu uhifadhi wa chakula, Waziri Mkuu alisema Serikali kupitia Wakala wa Taifa, hifadhi ya Chakula inaendelea kununua ziada ya mavuno yaliyopatikana kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kuyahifadhi.

"Sehemu ya hifadhi hiyo itatumika katika kuongeza upatikanaji wa chakula kwenye maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula hapa nchini" alisema.

Waziri Mkuu aliwaasa pia wananchi kutumia vizuri mavuno yaliyopatikana katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024 kwa kutunza chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya kwa kuzingatia kanuni bora za uhifadhi mzuri wa mazao ya chakula.

"Nitumie nafasi hii kuwakumbusha wananchi kuendelea kutumia chakula kilichopo sasa kwa uangalifu mkubwa, kuhifadhi chakula cha kutosha katika ngazi ya familia na kuepuka matumizi mabaya ya chakula au yasiyokuwa ya lazima," alisisitiza.

Kwa upande mwingine Waziri Mkuu alielekeza Wizara ya Kilimo kusimamia kwa ukaribu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu ujao wa kilimo.

"Wizara ya Kilimo isimamie kwa ukaribu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo hususani mbolea kwenye maeneo yote kwa kuzingatia jiografia za kanda za kilimo nchini," alisema.

Aliongeza kwamba, Wizara hiyo kupitia Maafisa Ugani wanalo jukumu la kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uhifadhi wa mazao.

"Maafisa Ugani wanapaswa kuendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uhifadhi wa mazao ya chakula na matumizi sahihi ya chakula katika ngazi ya familia," alisema.

# Dkt Mpango: Mabunge yana wajibu w




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mabunge Wanachama wa Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika uliofanyika Jijini Arusha.*

Na Debora Sanja

Zaidi ya Washiriki 280 kutoka Mabunge Wanachama wa Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika walishiriki katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 53 uliofanyika tarehe 1 hadi 6, Oktoba Jijini Arusha.

Washiriki wa Mkutano huo walitoka katika Mabunge 14 kati ya 19 wakiwemo Maspika wa Mabunge ya Kitaifa 10 pamoja na Manaibu Spika takribani 10 kutoka katika Mabunge ya Majimbo.

Akifungua Mkutano huo, Oktoba 3, 2024, Makamu wa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango alipongeza Kauli Mbiu ya Mkutano inayosema 'Mabunge ya Afrika kuwa Mstari wa Mbele katika Kupambana na Changamoto za Uhaba wa Chakula, Mabadiliko ya Tabianchi na Ajira kwa Vijana.'

Alisema kauli mbiu hiyo imekuja katika muda muafaka kwa kuwa changamoto hizo kwa sasa zimekuwa ni janga na tishio la utulivu wa kijamii na kiuchumi katika Bara la Afrika.

Alisema Mabunge ya Afrika ni vyombo muhimu katika kupambana na changamoto hizo ikiwemo kukuza haki za binadamu, demokrasia na utawala wa sheria.

Dkt. Mpango alisema kwa upande wa uhaba wa chakula, Mabunge ya nchi husika yanayowajibu wa kuhimiza uwekezaji katika kilimo ikiwemo kuongeza bajeti ya pembejeo za kilimo, kuboresha miundombinu na huduma nyingine.

"Kwa Tanzania, Bunge limekuwa likitunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kushughulikia uhaba wa chakula sambamba na Sera ya Taifa ya Kilimo, kipaumbele chetu ni kuwezesha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kufanya kilimo endelevu na kuwawezesha wakulima wadogo pamoja kutafuta masoko," alisema.

Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Dkt. Mpango alisema Mabunge na Wabunge wanao wajibu wa

# va Kuhimiza Uwekezaji katika Kilimo

kuhakikisha Serikali na wadau wengine wanachukua hatua madhubuti za kupambana na mabadiliko hayo na kwamba Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ikiwemo kutunga sheria za kutunza mazingira.

Akizungumzia tatizo la ajira, Dkt. Mpango alisema katika Bara la Afrika kila mwaka vijana milioni 12 hadi 13 wanaingia kwenye soko la ajira, lakini vijana milioni tatu tu ndio wanaopata ajira.

Alisema Mabunge ya Afrika yanapotekeleza majukumu yake ya kutunga sheria na kuishauri Serikali, yanapaswa kushirikiana na Serikali katika kukuza na kuendeleza sera za ajira pamoja na kubuni programu za kuwawezesha vijana kujiajiri.

Alisema pamoja na jitihada mbalimbali za kupunguza tatizo hilo, Tanzania imeongeza bajeti ya kilimo mara tatu zaidi katika kipindi cha miaka mitatu kwa sababu asilimia 75 ya Watanzania wanajihusisha na sekta ya kilimo.

Awali akizungumza katika ufunguzi huo, Spika wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson pamoja na kuwashukuru wajumbe wote wa mkutano huo, alimshukuru Mgeni Rasmi Dkt. Philip Mpango kwa kumwakilisha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuufungua mkutano huo.

Alitumia nafasi hiyo kuwashukuru wajumbe wa mkutano huo kwa kumuunga mkono na kumpigia kura katika uchaguzi wa nafasi ya Rais wa IPU.

Alisema CPA ni jukwaa muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge katika kukuza usawa wa kijinsia, haki za binadamu na utawala bora na kwamba katika mkutano huo wajumbe watakuwa na mijadala, warsha na vikao mbalimbali kwa kuzingatia malengo hayo.

Aliwataka wajumbe wa mkutano huo kuwapa kipaumbele wananchi wa nchi zao wanaowawakilisha katika mijadala wakati wote wa mkutano ili kuleta matokeo chanya katika maisha yao.

“Kwa pamoja tutayafanya Mabunge ya Afrika kuwa mstari wa mbele kwa kuwawezesha wananchi wetu kuwa na hali bora za maisha, kulinda mazingira na kuwatengenezea vijana kesho yao yenye tumaini na fursa,” alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa CPA Kanda ya Afrika ambaye pia ni Katibu wa Bunge la Tanzania, Ndugu Baraka Leonard alisema jumla ya Mabunge ya Kitaifa 14 na Mabunge ya Majimbo 12 yamehudhuria Mkutano huo.

Wengine waliozungumza katika Mkutano huo wa ufunguzi ni Rais wa CPA Kanda ya Afrika Mheshimiwa Segepoh Thomas Solomon, Mwenyekiti wa Kamati Tendaji wa CPA Afrika na Spika wa Bunge la Malawi Mheshimiwa Catherine Gotani Hara, Kaimu Mwenyekiti wa CPA Mheshimiwa Arthur Holder, Mheshimiwa Osei Kyei-Mensah-Bonsu Mjumbe wa CPA Afrika na Katibu Mkuu wa CPA Ndugu Stephen Twigg.

Ufunguzi wa Mkutano huo ulitanguliwa na vikao viingine ikiwemo vikao vya Kamati Tendaji ya CPA Kanda ya Afrika, Vikao vya umoja wa Makatibu Mezani pamoja na vikao vya kamati mbalimbali.

**Warsha ya Uwasilishaji Mada**

Katika Mkutano huo, vilevile kulikuwa na warsha ya uwasilishaji wa mada na majadiliano ambapo jumla ya mada 5 ziliwasilishwa kutoka Nchi ya Malawi, Ghana, Afrika ya Kusini, Namibia na Kenya na kuungwa mkono na wajumbe wengine.

Mada zilizowasilishwa ni pamoja na mada kuhusu “Maandalizi ya Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Bara la Afrika na Matumizi ya Vyanzo vya Nishati Mbadala Viwandani Katika Bara la Afrika: Mipango na Changamoto.

Mada nyingine ni Kuangalia Upya Mchango wa Wanawake Katika Mabunge, na Kurekebisha Mifumo ya Elimu Katika Bara la Afrika ili Kukabiliana na Ukosefu wa Ajira kwa Vijana Barani Afrika.

Aidha, mada ya tano ilihusu Maboresho ya Uchaguzi Katika Bara la Afrika ili Kukabiliana na Mzozo Unaoongezeka wa Kutokuwa na Imani na Taasisi za Kisiasa.

Mada hii iliwasilishwa na Mbunge wa Bunge la Afrika ya Kusini Mheshimiwa Bhekisizwe Hadebe na iliungwa mkono kwa andiko kutoka Bunge la Tanzania, lililowasilishwa na Mjumbe wa Kamati Tendaji ya CPA Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

Baadhi ya wachangiaji wa mada, ni pamoja na Spika wa Bunge la Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson na Mjumbe wa CPA Tawi la Tanzania Mheshimiwa Salome Makamba.

Akichangia mada hiyo, Mheshimiwa Spika pamoja na mambo mengine alijadili kuhusu changamoto ya watu kutojitokeza kwenda kupiga kura ikiwemo wanawake.

Kwa upande wake Mheshimiwa Makamba, alizungumzia kuhusu hatua zilichokuliwa na Tanzania za kufanya mabadiliko katika sheria za uchaguzi na sheria za vyama vya siasa kwa lengo la kumlinda mwanamke dhidi ya unyanyasaji wakati wa uchaguzi pamoja na kupunguza muda wa mashauri ya uchaguzi mahakamani.

Awali akichangia mada kuhusu

Maandalizi ya Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Bara la Afrika Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage alieleza jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoweza kuleta athari za kiafya kwa jamii.

Alieleza kuhusu umuhimu wa kuunganisha jitihada za kupambana na majanga na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu kupambana na majanga yanayotokana na athari za mabadiliko ya tabianchi

**Uchaguzi wa viongozi wapya**

Mkutano huo uliwachagua viongozi wapya wa CPA Kanda ya Afrika ambao ni Rais Mheshimiwa Jatta Fabakary Thombog ambaye ni Spika wa Bunge la The Gambia, Makamu Mwenyekiti wa Kamati Tendaji Mheshimiwa Abdul Sulaiman Marray-Conteh Mjumbe kutoka Sierra Leone na Mweka Hazina, Mheshimiwa Enos Asiimwe Mjumbe kutoka Uganda.

Vilevile Mkutano uliwapatia viongozi waolipita wa CPA Kanda ya Afrika tuzo maalum ya kutambua mchango wao.

Viongozi hao ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukas Sinimbo Muha, kutoka Namibia, Mweka Hazina Mheshimiwa Ntombi Mekgwe, Makatibu wa CPA Kanda, Stephen Kagaigai na Mheshimiwa Jaji Nenelwa Mwihambi, ndc, Mwakilishi Mwandamizi wa Kanda, Makali Mulu, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Wanawake wa CPA Mheshimiwa Dkt. Zainab Gimba na Mwenyekiti Msaidizi Kamati Ndogo ya Wanawake Mheshimiwa Kayanga Baroda.

CPA Kanda ya Afrika imekuwa ikifanya mikutano yake mikuu ya kila mwaka kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali kwa kuzingatia malengo ya kuanzishwa kwa umoja huo.

Lengo la kuanzishwa kwa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya Madola ni kuchagiza amani, demokrasia, uwajibikaji na haki za binadamu miongoni mwa nchi wanachama.

Mkutano huu wa CPA – Kanda ya Afrika ni jukwaa muhimu la kuwakutanisha washiriki mbalimbali kwa lengo la kujadili masuala yanayowahusu kwa kuzingatia malengo ya kuanzishwa kwake ." alisema.

Pamoja na kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka, CPA imekuwa ikiandaa semina na mafunzo kwa lengo la kubadilishana uzoefu na pia imekuwa ikiandaa machapisho mbalimbali.

CPA ilianzishwa mwaka 1911 ikiwa na Kanda tisa ikiwemo Kanda ya Afrika ambayo ina wanachama 19 wa Mabunge ya Kitaifa na 64 wa Mabunge ya Majimbo.




*Makamu wa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Umoja wa Mabunge Wanachama wa Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika mara baada ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Chama hicho uliofanyika Jijini Arusha.*

# Bunge laitaka Serikali kubadilisha umiliki wa Shamba la Malonje



*Mwenyekiti wa Kamati Maalum iliyoundwa na Spika wa Bunge kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na Vijiji vinavyolizunguka shamba hilo, Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya akiwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo Bungeni.*

*Na. Lawrence Raphaely*

Bunge limepitisha azimio la kuitaka Serikali kubadilisha umiliki wa Shamba lote la Malonje (Shamba la Efatha) lililopo katika Kijiji cha Sikaungu katika Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa kwa kuzingatia sheria na maslahi ya umma.

Azimio hilo lilipitishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita kufuatia taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na Vijiji vinavyolizunguka shamba hilo kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa.

Akizungungumza Bungeni wakati kuwasilisha taarifa ya Kamati Maalum juu ya uchunguzi wa mgogoro huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya alisema kupitia Azimio hilo la Bunge kuwa Serikali inapaswa iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane vinavyozunguka shamba pamoja na Gereza la Mollo utakaobainisha mahitaji ya ardhi pamoja na matumizi ya ardhi hiyo.

Alisema Serikali inapaswa kulipima shamba hilo na kuligawa upya kwa wahusika ambao ni wanavijiji, Gereza la Mollo, mwekezaji (Efatha) na wenye vitalu kwa kuzingatia mahitaji halisi ya ardhi kwa wanavijiji, uwezo wa Mwekezaji, uwezo wa wenye vitalu na mahitaji ya Gereza la Mollo.

Aidha kufuatia taarifa ya Kamati hiyo Bunge pia lilipitisha azimio la kuitaka Serikali isimamie utekelezaji wa kanuni zinazoweka ukomo wa wananchi kumiliki ardhi nchini.

Akisoma azimio ambalo hatimaye liliridhiwa na Bunge, Mhe. Manya alisema Serikali inapaswa isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya Mwaka 2007 kwa kupima ardhi ya nchi nzima na kuiwekea mipango na matumizi ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi, kuwezesha umiliki unaotambulika, jambo litakalowezesha ardhi ndogo kutumika kwa manufaa ya watu wengi na kupunguza migogoro ya mipaka na umiliki.

Kuhusu mgogoro katika shamba hilo la Malonje, Mheshimiwa Prof. Manya alisema mgogoro huo umekuwepo kwa muda mrefu na jitihada kadhaa zimefanyika katika kujaribu kutatua mgogoro huo.

"Pamoja na jitihada hizo, bado mgogoro umeendelea kuwepo. Tathmini ya jumla ya matokeo ya uchambuzi wa hadidu zote zilizotolewa kwa Kamati inaweza kujumuishwa kwa kuelezea kasoro mbalimbali kama chanzo cha mgogoro wa shamba la Malonje," alisema.

Aliongeza kuwa kasoro hizo zimebainika kwa pande zote ikiwemo Serikali, mwekezaji na wanavijiji huku suala kuu likiwa kujielekeza katika kuzingatia haki za raia katika matumizi ya ardhi.

"Kamati imependekeza kuanza upya kwa kufuta umiliki wa shamba lote la Malonje na kulipima upya pamoja na kuvipima upya vijiji vinavyozunguka shamba hilo

kwa maslahi mapana ya nchi," alisema.

"Lengo ni kufanya mgawanyo mpya kwa kuzingatia mahitaji halisi na kurekebisha kasoro mbalimbali zilizojitokeza awali. Ni matarajio ya Kamati kwamba, hatua hii itatamatisha migogoro katika shamba hilo na kurejesha amani na utulivu kwa wanakijiji pamoja na Mwekezaji," alisisitiza.

Katika azimio lingine Bunge pia liliazimia Serikali izielekeze mamlaka zinazohusika na uendeshaji wa kesi za jinai nchini zifanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kufuatia taarifa ya Kamati kuonesha kuwa kuna kila dalili za kuwepo kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu katika Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo na waliohusika katika tuhuma za vitendo hivyo hawajachukuliwa hatua zozote za kisheria.

Wakichangia kuhusu taarifa hiyo Waheshimiwa Wabunge walimpongeza Mheshimiwa Spika kwa hatua aliyochukua ya kuunda Kamati hiyo ambayo kufuatia uchunguzi waliofanya itasaidia katika kutatua mgogoro huo.

Kwa upande wa Mheshimiwa Festo Sanga alisema idadi ya watu nchini inaongezeka na mahitaji ya ardhi yanazidi kuongezeka kila siku na hivyo kuna kila sababu ya umiliki wa shamba la Malonje ukabatilishwa ili mchakato wa kuligawa upya ufanyike na ili wananchi waweze kupewa fursa ya kupata ardhi.

"Kwenye hili jambo la Malonje idadi ya watu nchini inaongezeka na mahitaji ya ardhi yanazidi kuongezeka kila siku. Kutokana na kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa ardhi hivyo tumependekeza kwamba umiliki wa lile shamba ubatilishwe ili tuweze kwenda kwenye mchakato wa kuligawa upya ili wananchi na wenyewe waweze kupata haki," alisema.

Naye Mheshimiwa Asia Halamga alisema dhumuni la shamba la Malonje kugawanywa kwa mwekezaji ilikuwa ni kwa ajili ya uwekezaji lakini alichokifanya ni kuchukua shamba na kutokwenda kwenye malengo na dhamira iliyokusudiwa.

"Madhumuni yalikuwa ni ufugaji ambao utawasaidia vijiji vya jirani ama wananchi wanaolizunguka shamba na kufanya Mkoa wa Rukwa kupitia Shamba la Malonje kuwa na kitega uchumi kupitia uwekezaji huo," alisema.

Aliongeza kuwa jambo la kushangaza na ajabu ni kwamba mwekezaji ambaye alikidhi vigezo alipopewa shamba hilo alifanya shughuli za kilimo na siyo ufugaji na wakati hata wananchi walikataliwa kufanya shughuli za kilimo badala ya ufugaji.

Kwa upande wake Mheshimiwa Innocent Bilakwate alisema kabla ya kuundwa kwa Kamati Maalum ya kuchunguza mgogoro huo wa ardhi wanachi walipata shida na mateso ya muda mrefu, hivyo kuundwa kwa Kamati hiyo ilikuwa ni faraja kubwa kwao.

"Hawa wananchi inaonesha wamepata shida, wamepata mateso muda mrefu, sasa Mungu ameamua, kupitia wewe Mheshimiwa Spika, aweze kumaliza mgogoro huu na naamini utaisha," alisema.

"Mheshimiwa Spika, kama walivyochangia watangulizi wenzangu, kwa kweli ukifika kule *site* ukawaona wale wananchi mateso ambayo wameyapata, umaskini walionao, namna ambavyo wananchi wamepigwa na kunyanyaswa, kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha sana. Tunapenda wawekezaji, lakini wawekezaji wa namna hii kwa kweli, Serikali iwaangalie kwa karibu," alisisitiza.

Kwa upande mwingine, akizungumza kuhusu taarifa hiyo ya Kamati Maalum, Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson alisema kwamba Waheshimiwa Wabunge ambao wana changamoto kama ambazo Kamati iliichunguza, wanaweza kuzungumza na Kamati ya Bunge ya Ardhi, ili Kamati kadiri inavyofanya kazi zake, Serikali inapoenda mbele yake, wataendelea kuifuatilia hiyo migogoro yote.

"Kwa sababu, hatutaweza kumudu kutengeneza Kamati, kwa ajili ya kila mgogoro na tunaamini kwa juhudi mbalimbali zinazoendelea kufanywa na Serikali, migogoro itaendelea kupungua na kisha kumalizika kabisa," alisema.

Kuhusu michango ya Waheshimiwa Wabunge katika taarifa hiyo ya Kamati Meshimiwa Spika alisema wanaruhusiwa kuchangia kadiri waonavyo na si sahihi kwamba wakati mwingine mchango wa Mheshimiwa Mbunge mmoja unaonekana ndiyo Bunge limesema.

"Nimeona nitoe huu ufafanuzi, ili isije ikaleta mkanganyiko huko nje ambavyo Mheshimiwa Mbunge mmoja akiwa amezungumza jambo fulani, basi inaonekana ni Bunge limesema. Ni mawazo yake na anaruhusiwa humu ndani, analindwa kabisa na Ibara ya 100 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa Bunge limeielekeza Serikali kuchukua hatua kadhaa kuhusiana na mgogoro huo, lakini hatua hizo zifuate utaratibu uliopo na pia, zifuate Sheria za nchi.

"Kwa hiyo, Serikali itakapomaliza mchakato wake,wote tutataarifiwa. Wakati huo, nawaomba wananchi kama ambavyo huko nyuma wameendelea kuwa watulivu na wastahimilivu, basi utulivu huo na ustahimilivu uendelee wakati Serikali inaendelea kujipanga kutekeleza maagizo haya ya Bunge," alisema.

Kwa upande wa Serikali akizungumza kuhusu taarifa hiyo ya Kamati, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa William Lukuvi alimpongeza Mheshimiwa Spika kwa hatua aliyochukua ya kuunda Kamati ya kuchunguza mgogoro huo na kuongeza kwamba Serikali itahakikisha inataekeleza maazimio ya Bunge.

"Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, lazima tutakuja kuripoti mwenendo na matokeo, yaani mwisho wa kazi hii ambayo tumeelekezwa na Bunge. Hatutasita kutekeleza mambo yote yatakayokuwa yameazimiwa na Bunge pamoja na hili," alisema.

# Bunge lapitisha Miswada Nane katika Mkutano wa 16

Na. Debora Sanja

Bunge limepitisha Miswada ya Sheria minane (8) katika Mkutano wa Kumi na Sita uliofanyika kati ya tarehe 27 Agosti hadi 6 Septemba, 2024.

Moja ya Muswada uliopitishwa na Bungeni ni Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024 ambao uliwasilishwa Bungeni na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa.

Katika Muswada huo pamoja na ilivyokuwepo ambapo wafanyakazi hao walikuwa wanatoka katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Vilevile TAA itakuwa na Bodi ya Wakurugenzi, Mamlaka ya Bodi, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na masuala mengine yanayohusu maofisa na watumishi wa mamlaka.

Muswada mwingine uliwasilishwa katika Mkutano huo wa Bunge, ni Muswada wa Sheria mahakama kufuta amri ya kuasili mtoto baada ya kupokea maombi ya mzazi, mlezi au ndugu.

Aidha, Bunge pia lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 ambao pamoja na mambo mengine umelenga kubadilisha masharti ambapo mwanachama wa mfuko atalipwa mafao bila kujali kama mwajiri amekamilisha kuwasilisha michango kwenye mfuko.



mambo mengine, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imepewa jukumu la kusimamia viwanja vyote vya ndege ikiwemo viwanja vidogo.

Awali TAA ilikuwa ikitekeleza jukumu hilo kama Wakala chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245 na kusimamiwa na Bodi ya Ushauri.

Muswada huo pia unaipa mamlaka TAA kuwa na wafanya kazi wake wa zimamoto tofauti na ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto wa Mwaka 2024 uliowasilishwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima.

Katika Muswada huo uliopitishwa na Bunge umeweka adhabu ya kulipa fidia kwa waathirika, kuanzisha mabaraza ya watoto na mahakama zao katika kila wilaya.

Aidha, umetoa mamalaka kwa Marekebisho hayo yalisomwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

Alisema pia marekebisho mengine ni kutoa uhuru kwa mwanachama kuchangiwa na mwajiri zaidi ya mmoja kwa ridhaa yake pamoja kumruhusu mwanachama ambaye hajafikia umri wa kustaafu kutumia sehemu ya mafao yake

kama dhamana kwa mkopo wa nyumba.

Muswada mwingine uliopitishwa ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 na uliwasilishwa Bungeni wa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi.

Mojawapo ya marekebisho yaliyofanyika ni pamoja na kuondoa sharti la kila muhitimu wa shahada ya sheria kulazimika kupitia na kufaulu masomo ya sheria kwa vitendo hata kama hakusudii kufanya kazi za uanasheria katika utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Profesa Kabudi, marekebisho hayo yamehusisha kifungu cha 5 ili kuongeza wigo kwa Shule ya Sheria kutoa mafunzo ya kozi nyingine maalumu za mafunzo ya sheria.

Kwa upande wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 pamoja na mambo mengine umelenga kuiwezesha Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani.

Muswada huo uliwasilishwa Bungeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Simbachawene.

Alisema lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha TAKUKURU kufanya kazi kwa ufanisi katika nyanja hizi na hivyo kuhakikisha uadilifu na haki vinadumishwa katika michakato ya uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha na tasnia ya burudani.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari, akizungumza Bungeni

Aidha, katika Muswada huo kuna kifungu kimeweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu mwenye mamlaka kuomba rushwa ya ngono au kuomba upendeleo wa aina nyingine kama sharti la kutoa au kupata ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

Pia kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu anayeahidi au kutoa rushwa ya ngono au upendeleo mwingine kwa mtu mwenye mamlaka au aliye katika nafasi ya mamlaka ili kumshawishi mtu huyo kutoa upendeleo wa ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

Katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 Bunge lilipitisha Muswada huo huku likifuta kifungu chenye sharti la lazima la wauzaji bidhaa au huduma kuonesha bei ya kila bidhaa au huduma na kuweka adhabu ya faini isiyopungua Shilingi 10,000 na isiyozidi Shilingi milioni moja ili kulinda walaji.

Muswada huo uliwasilishwa Bungeni na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo.

Muswada huo ulikuwa na vifungu 24 na hivyo Bunge limepitisha vifungu 23 na hicho kimoja Serikali imepewa muda zaidi wa kufanya utafiti.

Miswada mingine iliyopitishwa katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria (Na. 2) wa Mwaka 2024 iliyowasilishwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari.

# Dkt. Salema achaguliwa kuwa Mbunge wa EALA

Na. Zuhura Mtatifikolo

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilimchagua Mheshimiwa Dkt. Gladness Salema kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge.

Uchaguzi huo ulifanyika Septemba 5, 2024 Bungeni Jijini Dodoma ambapo Dkt. Salema alipata kura 254 kati ya kura 274 zilizopigwa.

Akitangaza matokeo hayo Bungeni, Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, alisema jumla ya Wabunge wote ni 393 lakini waliojitokeza kupiga kura walikuwa Wabunge 274.

Alisema kati ya kura 274 zilizopigwa, kura mbili ziliharibika, kura 18 zilikuwa za hapana huku kura za ndiyo zikiwa 254.

Mheshimiwa Zungu alimpongeza Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia mchakato mzima wa kumpata mgombea mwenye sifa zote zinazotakiwa.

"Nampongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa CCM Mheshimiwa Rais Dkt.Samia kwa kusimamia mchakato mzima wa kumpata mwakilishi wa EALA kwa haki na uwazi na amepatikana mtu bora zaidi miongoni mwa bora.

"Waheshimiwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, nawapongeza kwa kweli mmeonesha hekima, uelewa na kujua mgombea yupi tunayemtaka aende akalipambanie Taifa letu katika Afrika Mashariki, Mgombea huyu ameonesha ukomavu, siasa anazijua.Lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kumpigia kura nyingi za ndiyo," alisema.

Awali aliyekuwa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi, alisema mgombea huyo alikuwa anasifa zote za kuchaguliwa kuwa Mbunge wa EALA.

Alitaja sifa hizo ni kuwa awe raia wa nchi mwanachama wa Jumuiya, awe na sifa za kugombea ubunge wa jimbo, asiwe mtumishi wa Bunge la Afrika Mashariki na asiwe katika nafasi ya Waziri.

Akizungumza mara baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge Mteule, Mheshimiwa Dkt. Salema aliwashukuru Wabunge kwa imani waliyoionesha kwake huku akiahidi kufanya kazi kwa bidii.

"Naomba nimshukuru sana Rais wangu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini pamoja na chama changu cha CCM na viongozi wote, Kamati Kuu, Sekretarieti na Wajumbe wote. Pia naomba niwashukuru Wabunge wa Upinzani ninaamini wao pia wana imani na mimi"

"Ninasimama mbele yenu nikiwa na moyo wa shukrani kwa imani mliyonipa kwamba ninaweza kubeba dhamana ya Taifa hili, naahidi kufanya kazi kwa bidii," alisema.

Septemba 2 mwaka huu, Wabunge wa CCM walimchagua Mheshimiwa Dkt. Gladness Salema kuwa mgombea ubunge wa EALA kupitia chama hicho baada ya kupata kura 136.

Katika uchaguzi huo uliohusisha wagombea tisa, Dkt. Gladness Salema aliwashinda wenzake wawili alioingia nao katika upigaji kura awamu ya pili ambao ni Lucia Sebastian aliyepata kura, 52 huku Queenelizabeth Makune akipata kura 51.

Wagombea wengine ni Fatma Kange, Theresia Dominic, Prof. Neema Kumburu, Fatma Msofe, Hawa Nkwera na Maria Sebastian.

Uchaguzi huo ulifanyika kuziba nafasi kufuatia aliyekuwa Mbunge wa Afrika Mashariki, Shogo Mlozi, kufariki dunia Juni 13 mwaka huu.

Dkt. Gladness Salema tayari ameshaapishwa kuwa Mbunge wa EALA katika Mkutano wa Bunge hilo unaofanyika Kampala nchini Uganda.



# Misingi ya Utaratibu na Uen

Na Athuman Hussein, ndc
a.brambati@bunge.go.tz

Matoleo yaliyotangulia kabla ya Toleo la Saba yalifafanua adabu za uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Jumla ya adabu nane za uendeshaji wa Vikao vya Bunge zimekwisha fafanuliwa. Kwa kukumbushia adabu hizo ni kujadili Hoja moja hadi ikamilike, kuelekeza mjadala kwenye ustahili wa Hoja na maoni ya wengi yazingatiwe huku ya wachache yakisikilizwa.

Adabu nyingine ni Mbunge kutoanza kuzungumzia hoja inayojadiliwa kabla ya kutambuliwa na kuitwa kuwa mzungumzaji. Hoja hizo zote zilijadiliwa kabla ya Toleo la Saba la Jarida hili. Mwendelezo wa adabu za vikao vya Bunge ulijitokeza kwenye Toleo la Saba ambapo adabu zaidi zilifafanuliwa.

Adabu zilizoelezewa katika Toleo la Saba ni kujadili Hoja na kuacha kujadili mtu aliyejadili Hoja awali. Nyingine ni kuelekeza mjadala kwenye ustahili wa pendekezo kwa kuepuka mambo yasiyotakiwa. Vilevile adabu inayohusu misingi stahiki ya utoaji wa nafasi kwa Wabunge kuchangia hoja na adabu inayohusu kurahisisha ufikiaji wa uamuzi kwenye vikao.

Upekuzi wa Kanuni za Kudumu za Bunge umefanyika kueleza namna Bunge la Tanzania linavyozingatia misingi ya uedneshaji wa Vikao vya Bunge. Ikumbukwe kuwa mtiririko wa maudhui juu ya utaratibu na uendeshaji wa Vikao vya Bunge ulijengwa kwenye chimbuko lake kwa hapa tulimrejea Meja wa Jeshi la Marekani aliyejulikana kwa jina la Meja Henry Martyn Robert. Bwana huyu alisukumwa na hali ya wachangiaji, ubora na staha ya majadiliano na ufanisi wa mchakato wa majadiliano ili kupata uamuzi bora. Hayo yalibainika kwa kurejea Toleo la Kanuni za Robert Toleo la mwaka 1876 na nyongeza za adabu zilizochomoza kulingana na maendeleo ya



Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, akiongoza kikao cha Kamati ya U

ya uendeshaji wa vikao alivyo hudhuria ambavyo havikuwa na adabu maalum za mjadala au majadiliano.

Msukumo huo ulimfanya achapishe Toleo la Kwanza la Kanuni za Robert kuhusu utaratibu *(Robert Rules of Order)*. Kimsingi kanuni za Robert zililenga haki tamaduni za kibunge duniani.

Katika matoleo baada ya toleo la saba, muendelezo utafanyika kwa kuangalia mchakato wa hoja Bungeni tangu inavyoanza, inavyotambulishwa hadi uamuzi unavyofikiwa. Mtindo wa ufafanuzi utaendelea kuanza na maelezo ya jumla, rejea ya utaratibu wa

# ndeshaji wa Vikao vya Bunge

Bunge la Tanzania na ujenzi wa mazingatio.

Mahsusi kwa toleo hili, makala hii inafafanua dhana na aina za hoja Bungeni. Kwa kuanzia, ufafanuzi kuhusu maana ya "hoja" ni muhimu kwa kuwa ndilo wa kibunge, "hoja" ni pendekezo rasmi linalotolewa na Mbunge Bungeni kwamba, Bunge liamue jambo fulani. Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimetafsiri hoja kuwa ni pendekezo linalotolewa na Serikali, Kamati au Mbunge ili



Uongozi kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge Jijini Dodoma

jambo kuu. Kilugha, neno 'hoja' ni maelezo yenye msingi na vigezo vinavyothibitisha ukweli au uthabiti wa jambo. Maana nyingine ya neno 'Hoja' ni maoni au mapendekezo anayoyatoa mtu kwenye Mkutano, Kamati, baraza, Bunge au Serikali.

Kiistilahi, na hasa kwenye uga lipate uamuzi wa Bunge.

Katika desturi za kibunge, hoja huainishwa katika makundi makuu mawili. Hoja kuu *(main motion)* na hoja za pili *(secondary motion)*. Hoja kuu ni pendekezo rasmi linalowasilishwa na Mbunge ambalo likipitishwa linakuwa uamuzi au azimio la Bunge. Hoja ya aina hii hutolewa wakati wa mjadala pale ambapo hakuna shughuli nyingine inayosubiri.

Hoja za pili *(secondary motion)* ni jumla ya mapendekezo yanayotolewa na Mbunge au Wabunge wakati wa mjadala ili kurekebisha au kubadilisha jambo katika hoja kuu au uamuzi wake. Hoja za pili hutolewa wakati hoja kuu ikiendelea ili kusaidia katika kupangilia, kurekebisha au kuchelewesha uamuzi.

Kwa ufafanuzi zaidi, hoja za pili nazo hugawanyika katika makundi matatu. Hoja ndogo (*subsidiary motion*), Hoja zenye hadhi maalum (*privileged motion*) na hoja za kawaida (*incidental motion*). Hoja ndogo ni pendekezo linalotolewa na Mbunge kwa lengo la kurekebisha namna Hoja kuu inavyoshughulikiwa mfano, marekebisho au kuahirisha Hoja kuu.

Hoja zenye hadhi maalum ni pendekezo linalolenga masuala ya dharura ambayo hayahusiani mojakwa moja na Hoja kuu lakini yanahitaji kushughulikiwa mara moja. Kwa mfano, Hoja ya kuahirisha kikao au kuweka muda wa kikao kijacho, ina hadhi maalum katika mpangilio wa hoja.

Aina ya tatu ya hoja za pili ni hoja za kawaida. Hoja za aina hiyo hujitokeza wakati Bunge likiendelea na majadiliano. Katika

maendeleo ya majadilani, hoja hizi ni lazima zishughulikiwe mara moja. Mfano wa hoja hizo ni: kukumbusha utaratibu, *(point of order)*, na kutoa taarifa *(point of information)*.

Aina zote hizo za hoja zimezingatiwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inaweka mazingira yanayoruhusu hoja kutolewa. Masharti ya Kanuni hiyo yanagusa mfumo wa maneno ya Hoja na namna ambavyo Hoja inaweza kutokubaliwa.

Hoja kuu katika Kanuni za Bunge la Tanzania ndiyo yenye masharti mahsusi ambayo yanahusu vigezo, madhumuni yanayostahili na yasiyostahili, utaratibu wa kutoa notisi ya hoja, maneno yanayotumika katika hoja na mengine kuhusiana na hayo. Kwa mfano, hoja kuu zinaandikwa kwa kutumia mfumo wa vifungu vya maneno vya aina kuu mbili. Aina ya kwanza ni kifungu usuli *(preamble clause)* na ya pili ni kifungu azimio *(resolution clause)*.

Kifungu usuli kwenye hoja hueleza tatizo, shaka, wasiwasi, suala, msingi wa jambo, ukweli uliopo au hali ya jumla. Maelezo hayo hulenga kushawishi uamuzi wa Bunge, hivyo hutumia kifungu 'KWA KUWA'…, na pia 'NA KWA KUWA'… . Mfano wa hoja ni: KWA KUWA, suala la ukosefu wa vifaa vya afya vijijini limechangia kushuka kwa afya na ustawi wa wananchi, 'NA KWA KUWA' jitihada za awali za kuboresha huduma za afya katika maeneo ya vijijini, hazijatosheleza mahitaji yanayoongezeka, … .

Baada ya kifungu usuli, kipo pia kifungu azimio (*resolution clause*). Kifungu azimio kwenye hoja kuu kinabainisha hatua au uamuzi wa Bunge kuhusu jambo linalopendekezwa. Kifungu hiki kinaundwa kwa maneno 'KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, …'.

Kwa kawaida sehemu hii ya hoja (Kifungu azimio) hubainisha hatua inayotakiwa, uamuzi unaokusudiwa, mamlaka inayohusika namuda ikiwa itafaa. Hoja kuu yenye vifungu hivyo inaweza kuwa imewekwa katika lugha ambayo italiwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 (3) ya Kanuni za Bunge.

Mfano wa Hoja kuhusu ukosefu wa vifaa vya afya vijijini unaweza kuwa kwamba, KWA KUWA, suala la ukosefu wa vifa vya afya vijijini limechangia kushuka kwa afya na ustawi wa wananchi, NA KWA KUWA, jitihada za awali za kuboresha huduma za afya katika maeneo ya vijijini hazijatosheleza mahitaji yanayoongezeka, KWA HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia ukosefu wa vifaa vya afya na kuripoti Bungeni hatua za zinazofikiwa katika utekelezaji, wakati wa Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge.

Kwa upande wa hoja za pili, Kanuni za Bunge la Tanzania zimetambua pia hoja hizo. Kanuni ya 62 (3) imetambua hoja zenye hadhi maalum zikiwemo: kutengua Kanuni; kuahirisha Bunge: kuahirisha mjadala; kutaka wageni waondoke Bungeni; kuahirisha shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura na hoja ya jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge. Utaratibu wa hoja hizo umewekewa masharti tofauti na hoja kuu.

Hoja nyingine ni hoja ya kutaka ombi lililowasilishwa Bungeni lijadiliwe, kuahirisha Shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura, hoja kuhusu haki za Bunge na hoja ya kutaka hati iliyowasilishwa Bungeni ijadiliwe. Hoja hizo kwa ujumla wake zinakuwa hazinasibiani na mjadala unaoendelea. Kwa kawaida, hoja hizo zinahusu mambo ya kufanyiwa kazi haraka, mambo ya dharura *(matters of immediate)* mambo yenye umuhimu wa kipaumbele *(overriding importance)* ambayo yanastahili kuingilia shughuli iliyokuwa ikiendelea.

Lengo la kuruhusu hoja zenye hadhi maalum ni kuwezesha uamuzi wa haraka wa Bunge. Mambo yanyoguswa katika hoja za iana hii na ambayo yanahitaji uamuzi wa haraka wa Bunge yametajwa na waandishi wa utaratibu wa kibunge ambao ni Robert III na wenzake katika kitabu chao: Robert Rules of Order, Newly Revised 12 Edition, Toleo la mwaka 2020.

Kwa kuweka Hoja zenye hadhi maalum kwenye utaratibu wa Kibunge, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaendana na utamaduni wa Kibunge duniani. Mantiki hasa ya Hoja za aina hiyo, ni kuruhusu Bunge liendeshwe kwa namna ambayo inajali umuhimu wa

kushughulikia masuala ya dharura yanayohusiana na uendeshaji, utaratibu au haki za Bunge. Masuala hayo yanastahili kupewa umuhimu na kipaumbele. Sababu ni kuwa, kufanya hivyo, kunawezesha uendeshaji bora wa kikao kwa kupata hatua stahiki kuhusu mambo ya dharura ya kiutaratibu, kiutawala au shida ya kukosewa kwa misingi ya utaratibu.

Sababu ya pili ya kuwa na hoja zenye hadhi maalumu katika utaratibu wa Bunge ni kuwezesha uendeshaji wa Vikao vya Bunge unaofaa na wenye ustahili kwa Kanuni za Bunge kuruhusu Hoja zenye hadhi maalum, inawawezesha Wabunge kupata fursa ya kubainisha mambo yanayowatia mashaka na kuwafanya wawe na wasiwasi ambao kama hautapatiwa ufumbuzi, inaweza kuvuruga ufanisi wa Bunge.

Sababu ya tatu ni kulinda haki maalum na hadhi za Wabunge. Hoja hizo zinapojitokeza na kuruhusiwa zinasaidia kunusuru haki maalum za Kibunge zinazoelekea kuvunjwa au zinazovunjwa zihifadhiwe. Hadhi, heshimia na haki maalum za Mbunge au Bunge zinapokuwa hatarini kuvunjwa zinahitaji afua (*intervention*) ya Bunge lenyewe kwa haraka. Hivyo, Hoja zenye hadhi maalum zinasaidia mahitaji hayo.

Sababu ya nne ni kuthamini umuhimu wa utaratibu wa Bunge unaostahili kuzingatiwa. Hoja zenye hadhi maalum zinawezesha mijadala kuendelea kwa utaratibu stahiki. Kwa mfano, hoja ya kuahiirisha Bunge au mjadala inapotolewa ikiwa Kikao cha Bunge kinaendelea kwa muda mrefu au wakati ambapo Wabunge wanahisi kuendelea na mjadala hakutakuwa na manufaa, inasaidia Kikao kuendeshwa wka utartibu bora.

Sababu ya tano ni ufanisi katika uamuzi wa Bunge. Kwa kuruhusu masuala yenye umuhimu zaidi kupewa kipaumbele, Kanuni za Bunge zinawezesha Bunge kuzingatia mambo muhimu inavyostahili. Hoja zenye hadhi maalum zinazingatia dharura na uharaka wa kushughulikia masuala yenye asili hiyo. Kwa namna hiyo, utaratibu huu unatoa nafasi ya kuondoa wasiwasi na mashaka yanayojitokeza kwa Wabunge hivyo, kuwezesha ufanisi katika uendeshaji wa vikao vya Bunge kutokana na kuwezesha Wabunge kujikita kwenye mjadala baadfa ya kuondokewa na wasiwasi.

Aina nyingine ya hoja ni hoja ndogo, hoja hiyo ni pendekezo linalotolewa na Mbunge kwa lengo la kurekebisha au kuboresha hoja kuu inayojadiliwa. Kwa asili hoja hii haijitegemei bali inategemea hoja kuu. Kwa mfano, wakati Bunge likijadili hoja kuu kama vile hoja ya Kamati, Mbunge yeyote anaweza kupendekeza marekebisho. Mfano fafanuzi unaweza kuwa kwamba, katika hoja kuu, Kamati inapendekeza mambo matatu: kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato, kufanya mapitio ya matumizi na kupunguza misaada isiyo na tija. Kwa hoja hiyo, Mbunge anaweza kutoa hoja ndogo ambayo inapendekeza marekebisho.

Katika hilo, Mbunge anaweza kupendekeza kuwa pendekezo la kupunguza misaada lisomeke: kutoa misaada isiyotakiwa kwa mujibu wa sheria na kutokutoa misaada yenye taswira ya kutokuwa na tija. Umuhimu wa hoja ndogo kama hiyo ni kuwezesha mjadala wa kina, kuongeza kina cha uchambuzi na uchanganuzi pamoja na kuweka mazingira kwa Bunge kupokea maelezo mapya yanayoongeza utoshelevu kwenye hoja, ili upatikane uamuzi ufaao.

Katika maelezo hayo, msisitizo hadi hapo ni kukumbuka kuwa majadiliano Bungeni yanaelekezwa kwenye hoja kwa namna inayozingatia adabu za mijadala ya Bunge. Kinachojadiliwa ni mapendekezo yanayotolewa kwa Bunge ili liamue. Mapendekezo hayo kwa istilahi za kibunge hujulikana kwa neno 'hoja'.

Katika Toleo hili, fasili ya neno hoja imetolewa na ufafanuzi na aina zake zimebainishwa kuwa ni hoja kuu, hoja zenye hadhi maalum na hoja ndogo. Toleo lijalo litaendeleza makala hii kwa mifano ya aina mbalimbali za hoja na kuonesha mchakato wa hoja katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msingi wa maelezo na ufafanuzi huo ni umuhimu wa kueleweka kwa taratibu na desturi za Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kinachopaswa kufuatiliwa na watu wake.

# Mfahamu Spika wa



*Mhe Abdulkarim Karimjee akitoa hotuba ya kuliaga Bunge la Tanganyika mwaka 1962.*

Na. Abdallah S. Hancha

Spika wa Bunge ndiye Kiongozi Mkuu wa moja ya mihimili mitatu ya Dola uitwao Bunge. Spika husimamia na kuliongoza Bunge ili kufikia maamuzi ipasavyo kwa kazi zilizowekwa bayana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na pia kwa kuzingatia Kanuni za Bunge. Yeye huadibu pindi Mbunge anapofanya mambo kinyume na kanuni za Bunge. Spika ndiye msemaji wa Bunge katika shughuli za kitaifa au shughuli nyingine zozote. Kila unapofanyika Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge, Jambo la kwanza linalofanyika baada ya Rais kuliitisha Bunge huwa ni kumchagua Spika wa Bunge.

Kihistoria, Bunge la Tanzania limeongozwa na Maspika Kumi kwa maana watatu waliongoza wakati wa Baraza la Kutunga Sheria na saba wakaongoza Bunge la Tanzania. Maspika watatu waliongoza Baraza la Kutunga Sheria ni: Mhe. Brigedia William Scuphum, Mhe Sir John H. B. Nihill na Mhe. Abdulkarim Y. A. Karimjee. Maspika walioliongoza Bunge la Tanzania ni: Mhe. Chifu Adam Sapi Mkwawa; Mhe. Chifu Erasto Mbwana Mang'enya; Mhe. Pius Msekwa, Mhe. Samuel John Sitta; Mhe. Anne Semamba Makinda; Mhe. Job Yustino Ndugai; na Mhe. Dkt. Tulia Ackson.

Mhe. Spika Abdulkarim Karimjee yeye aliliongoza Baraza la Kutunga Sheria na kuendelea na nafasi hiyo baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 lilipoundwa Baraza la Taifa la Tanganyika kabla ya kubadili jina na kuitwa Bunge la Tanganyika mwaka 1962.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania historia yake inaanzia Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika lililoanzishwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge la Uingereza mwaka 1926 iliyoitwa "*The Tanganyika (Legislative Council) Order in Council,* 1926" tarehe 19 Machi, 1926. Gavana aliyekuwa akitawala kipindi hicho kwa niaba ya Malkia wa Uingereza, Sir Donald Cameron aliteua wajumbe 20 wa Baraza hilo lililozinduliwa tarehe 10 Oktoba, 1926 na kikao cha kwanza cha Baraza hilo kilifanyika Dar es Salaam tarehe 07 Desemba, 1926 na yeye akawa Mwenyekiti wa Baraza hilo. Gavana aliendelea kuliongoza Baraza hilo kwa takriban miaka 27. Mwaka 1953, yalifanyika mabadiliko ambapo Gavana alikoma kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Kutunga Sheria na badala yake Spika akawa ndiye kiongozi wa Baraza. Spika wa Kwanza wa Baraza la Kutunga Sheria akawa Brigedia William E. H. Scupham aliyeapishwa tarehe 1 Novemba 1953. Spika aliyefuata alikuwa Sir Barclay Nihill kabla ya Spika Adulkarim Karimjee kushika hatamu na kuliongoza Baraza kuanzia mwaka 1959 na kuendelea na cheo hicho hata baada ya Uhuru wa Tanganyika lilipoanzishwa Baraza la Taifa la Tanganyika. Mhe Abdulkarim aling'atuka nafasi ya Spika mwaka 1962 wakati wa Bunge la Tanganyika.

Mhe. Abdulkarim aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika mwaka 1949. Aliendelea kuwa Mjumbe wa kawaida hadi mwaka 1954 alipochaguliwa kuwa Naibu Spika. Kumuimarisha na kumuandaa kuwa Spika, Mhe Abdulkarim alialikwa mwaka 1956 na Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Parliamentary Association)* kwenda kushiriki mafunzo ya vitendo ya kibunge *(Parliamentary Procedure and Practice)* kwa mwezi mmoja. Katika mafunzo hayo, alionesha uhodari mkubwa wa mafunzo aliyopatiwa akiwa Uingereza. Weledi na maarifa aliyoyapata akiwa mafunzoni, yalimwezesha kuliendesha vema Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika mwishoni mwa mwaka 1957 na mwaka 1958

# a Kwanza Mzalendo

alipokaimu nafasi ya Spika baada ya Spika Sir William Scupham kutohudhuria vikao kutokana na sababu mbalimbali.

Mhe. Abdulkarim alichaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika mwaka 1959. Wakati harakati za kudai Uhuru zikiendelea, naye kama Spika alikuwa karibu na Mwl. Julius K. Nyerere katika hatua zote za kudai uhuru wa Tanganyika. Baada ya Tanganyika kuwa huru, Mhe. Abdulkarim alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Tanganyika lililokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1961 katika ukumbi wa Karimjee. Hivyo, Mhe Abdulkarim akawa ni shuhuda wa mabadiliko ya kibunge kutoka Wabunge au Wajumbe waliokuwa wakiteuliwa hadi Wabunge wa kuchaguliwa wa Bunge la Tanganyika. Idadi ya Wabunge wa Bunge la Kwanza alililoliongoza walikuwa ni 81. Hivyo yeye akawa ndiye Spika wa kwanza mzalendo baada ya Uhuru wa Tanganyika. Mhe Karimjee alistaafu Spika mwaka 1962. Mhe. Abdulkarim anakumbukwa kwa kuziongoza vyema sherehe za uhuru wa Tanganyika mwaka 1961. Amewahi kutunukiwa Udaktari wa Heshima na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1973.

Mhe. Abdulkarim amewahi kuwa Meya wa Jiji la Dar es salaam mara tatu. Mara ya kwanza alichaguliwa kuwa Meya mwaka 1951, Mara ya pili ilikuwa ni mwaka 1954, alishika cheo hicho kwa mara ya tatu mwaka 1957. Aidha, aliwahi kuwa Naibu Meya mara mbili kwa maana ya mwaka 1952 na mwaka 1956. Mhe. Abdulkarim aliheshimika sana kwa utumishi wake uliotukuka na jinsi alivyojitoa kuisaidia jamii. Mathalan, akiwa Meya alimshawishi baba yake Sir Yusufali Karimjee wajenge jengo kwa ajili ya ofisi na kumbi za mikutano kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dar es salaam. Baba yake aliafiki hoja hiyo na kuamua kujenga jengo hilo na kulikabidhi kama zawadi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dar es salaam mwaka 1955. Jengo hili limewahi kutumiwa na Bunge kabla na baada ya uhuru kwa muda mrefu mpaka Bunge lilipohamia Dodoma. Utumishi wake ulitambulika vema hata nje ya mipaka na hivyo Mhe. Abdulkarim akatunukiwa cheo cha heshima na Serikali ya Uingereza kiitwacho Kamanda wa Himaya ya Muingereza *(Commander of the British Empire - CBE)* kwa ajili ya huduma alizokuwa akitoa kwa jamii.

Aidha, Mhe. Abdulkarim amewahi kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), na pia Benki ya Taifa ya Biashara (NBC). Vilevile, amewahi kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia mwaka 1961 hadi mwaka 1970.

Mhe. Abdulkarim alikuwa ni mtu anayependa kusoma na kutaka jamii ijielimishe ili iweze kuendelea na kufikia malengo inayojiwekea. Kutokana na maono hayo, aliweza kuratibu ujenzi wa Maktaba Kuu ya Taifa (Tanganyika Central Library). Katika mchakato huo wa kuhakikisha maktaba kuu inapatikana, yakafikiwa makubaliano kwamba familia yake ichangie Paundi 65,000 na Serikali itoe kiasi sawa na hicho kwa ajili ya kufanikisha ujenzi huo. Jambo hilo lilitekelezwa ipasavyo na kwa uangalizi wa Mhe Adulkarim, maktaba iliyokusudiwa ikajengwa.

Pamoja na kuwa mtumishi wa Serikali, Abdulkarim alikuwa ni mfanyabiashara na pia mkulima wa mashamba makubwa ya mkonge, kahawa na chai. Aidha alikuwa na biashara za ujenzi wa nyumba za kupangisha. Aliweza pia kupata leseni ya kuwa wakala wa magari ya kampuni ya Toyota kutoka kampuni inayozalisha magari hayo *Toyota Motor Corporation.* Magari haya yalipendwa na wengi na hivyo alifanikiwa kufanya biashara nzuri iliyompa utajiri mkubwa.

Abdulkarim Yusufali Karimjee alizaliwa Zanzibar tarehe 15 Februari, 1906. Alipata mafunzo ya elimu ya msingi kwa lugha za Gujarati na kiarabu Zanzibar. Baada ya kumaliza elimu ya msingi, mwaka 1917 alipelekwa Burhangpur, India kwa ajili ya kusoma kiingereza kwa miaka miwili na kurejea Afrika mwaka 1917 akiwa na miaka 13 kutokana na sababu za kiafya. Mwaka 1919 akawa ni mwanafunzi katika ofisi kuu ya familia yake jijini Dar es salaam chini ya uangalizi wa Akberali Adamjee aliyekuwa meneja kwa wakati huo.

Mwaka 1930, Abdulkarim Karimjee alimuoa Bi Batool Noorbhai Jafferijee kutoka Karachi, Pakistan na kujaaliwa kupata Watoto wawili wa kike. Abdulkarim na mkewe waliamua kuishi Dar es Salaam ambako ndipo alipoanzia kufanya kazi akiwa ni msimamizi wa Idara ya Uagizaji na Uuzaii wa bidhaa (Import/Export Department) hasa za kilimo. Kutokana na kazi hii alitembelea sehemu mbalimbali ulimwenguni kama Ujerumani, Uingereza, Uswisi, Ufaransa, India na Hispania.

Miaka 1970 akiwa anajishughulisha na kazi zake nyumbani kwake Dar es salaam, Mhe. Abdulkarim alianguka na kupata maumivu kidogo. Akasafiri kwenda London na akiwa huko akalazwa katika Hopitali iitwayo *Princess Grace Hospital*. Hali haikuwa nzuri hivyo tarehe 7 Septemba, 1977 akahamishiwa hospitali nyingine iitwayo *Royal Free Hospital* kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Wakati akisubiri kufanyiwa uchunguzi wa afya yake, akapata mshituko wa moyo na kufariki dunia. Alizikwa tarehe 9 Septemba, 1977 hukohuko London katika makaburi ya Brookwood.

# Usimamizi wa Kibunge wa M

Na Athuman Hussein, ndc
a.brambati@bunge.go.tz

Makala hii inayoendelea inapokea mwishilizo kwenye Toleo la Saba ambalo lilifafanua nasaha za Benki ya Dunia kuhusu uendeshaji wa Kamati za Usimamizi wa fedha za umma. Nasaha hizo zimebainisha vigezo vitatu vilifafanuliwa na kigezo kimoja kikaelezwa kinavyojitokeza kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwendelezo katika toleo hili unabebwa na mawazo ya Mwanafalsafa wa Kichina anayesadikiwa kuishi takribani karne ya 6 kk. Jina lake ni Lao Tzu mwenye mawazo kwamba, 'safari ya maili elfu moja huanza kwa hatua moja'. Falsafa hii inashajiisha wasomaji na kuwaonesha kuwa kidogo kidogo hatua kubwa inafikiwa tangu kuanza kwa makala hii.

Matoleo yaliyopita kwenye safu ya usimamizi wa kibunge wa fedha za umma, yaligusia maana ya usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma, muundo wake na ngazi za usimamizi huo. Katika Toleo la Saba nasaha za Benki ya Dunia kuhusu Kamati za Kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma zilianza kupimwa katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Nia ni kutathmini uzingatiaji wa viwango na vigezo vya kibunge vinavyokubalika kimataifa vya uendeshaji wa Kamati zinazosimamia moja mwa moja matumizi ya fedha za umma.

Hatua iliyofikiwa kiufafanuzi ni kubwa kwa wasomaji wanaofuatilia safu hii. Hatua hiyo sasa inaendelezwa kwa kufafanua vigezo vingine viwili vitokanavyo na nasaha za Benki ya Dunia. Kigezo kimoja kilichofafanuliwa ni ushiriki wa waziri katika Kamati ya Bunge yenye jukumu la kuanangalia hesabu zinazohusika na matumizi ya fedha za umma. Katika makala hii kigezo cha uwakilishi wa kambi za vyama vya siasa Bungeni na ushirikiano wa kambi hizo vinachunguzwa katika Kanuni za Bunge.

Kwa kuanzia, Kanuni ya 135 (3) ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti kwamba, Wajumbe wa Kamati zote watateuliwa na Spika kwa namna inayowezesha kila Mbunge kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati mojawapo ya Kamati za Kudumu za Bunge. Kanuni ya 135 (5) ya Kanuni za Bunge imeainisha vigezo vinne anavyozingatia Spika wakati wa kuteua wajumbe wa Kamati za Bunge.

Miongoni mwa vigezo hivyo ni uwiano kwa kuongozwa na asilimia ya uwakilishi ilivyo Bungeni. Kwa masharti hayo, Spika analazimika kuzingatia uwakilishi wa vyama vya siasa Bungeni katika idadi ya wajumbe wa kila Kamati ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia matumizi ya fedha za umma. Kamati hizo ni Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Uwakilishi wa vyama vya siasa Bungeni umezingatiwa katika orodha ya wajumbe wa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Miongoni mwa wajumbe wa Kamati hizo, wapo Wabunge ambao wanatoka miongoni mwa Wabunge walio wachache Bungeni. Uwakilishi huo unaendana na nasaha za Benki ya dunia. Bunio katika nasaha za Benki ya Dunia ni kuwa uzingatiaji wa uwakilishi wa vyama vya siasa katika Kamati hizo, unaweka uhakika wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Inaaminika kwamba, wajumbe walio wachache Bungeni hawana maslahi sawa ya kisiasa na wabunge walio wengi linapojitokeza suala la matumizi ya fedha za umma. Tofauti hiyo inachukuliwa kuwa inapunguza hatari ya upendeleo wa kisiasa na kukuza usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Kigezo kingine muhimu ni uongozi wa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma kuwa chini ya Wabunge wanaotokana na Kambi ya walio wachache Bungeni. Msingi wa kimtazamo katika kigezo hiki ni imani kwamba, Kambi ya walio wachache Bungeni ipo katika nafasi nzuri ya kusimamia matumizi ya fedha za umma kutokana na maslahi yake kwenye eneo hilo ikilinganishwa na kambi ya walio wengi.

Aidha, inaaminika kuwa, uongozi unaotokana na kambi ya walio wachache utaweka umuhimu kwenye ushawishi dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za umma kuliko uongozi unaotokana na kambi ya walio wengi Bungeni. Mtazamo huo ndio unaosukuma kuona kuwa, uongozi wa Kamati hizo ukitokana na Wabunge walio wachache Bungeni, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma, utaonekana kuwa upo.

Kwa msingi huo, masharti ya Kanuni ya 135 (10) ya Kanuni za Bunge yameruhusu Mbunge yeyote ambaye ni Mjumbe kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge. Masharti hayo kwa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma yametofautishwa na kuweka sharti mahsusi kwa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Kanuni ya 135 (11) ya Kanuni za Bunge, inataka wenyeviti wa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma watokane na wajumbe ambao ni wabunge miongoni mwa walio wachache Bungeni.

Kwa ujumla wake, Kanuni za Bunge la Tanzania zimechukua vigezo vyote vitatu vinavyotokana na nasaha za Benki ya Dunia kuhusu Kamati za Bunge

# Matumizi ya Fedha za Umma

zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Vigezo hivyo ni Mawaziri kutokuwa wajumbe wa Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma, uwakilishi wa kambi ya walio wachache Bungeni kwenye Kamati hizo na uongozi wa Kamati kuwa chini ya miongoni mwa Wabunge walio wachache Bungeni.

Baada ya ufafanuzi huo, makala hii inaendelea kwa ufafanuzi wa dhana kuu tatu kwa mnasaba wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Dhana hizo ni mamlaka, madaraka na majukumu ya Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma katika dhana ya Bunge kusimamia matumizi ya fedha za umma.


Kwa madhumuni ya kuthaminisha ufafanuzi huu, imelazimu kuonesha ombwe lililopo kiuelewa. Maelezo yanatolewa kwa kuzingatia mkanganyiko wa dhana kuu tatu kuhusu Kamati za Bunge katika usimamizi wa fedha za Umma. Kwenda pamoja na mtiririko wa maudhui, inaweza kufaa iwapo dhana hizo: mamlaka, madaraka na majukumu ya Kamati, zitaeleweka ipasavyo. Kwa kuanzia tuchukue maneno mamlaka, madaraka na majukumu kilugha.

Neno 'mamlaka' linaweza kuwa uwezo au haki ya kutoa amri (Kamusi kuu ya Kiswahili, Toleo la Tatu, ukurasa wa 578). Kwa maana hiyo kiistilahi, mamlaka ya Kamati ya Bunge ni uwezo au hali ya Kamati kutoa amri katika mawanda ya kazi yake. Vilevile, neno 'mamlaka' lina maana ya 'amri au uwezo wa juu wa kuongoza jambo'. Kwa fasili hiyo, mamlaka ya Kamati ni uwezo wa juu wa kuongoza jambo katika mawanda ya kazi yake.

Kwa desturi za kibunge, Kamati za Bunge hazina mamlaka, isipokuwa kuhusu utaratibu wake tena kwa masharti ya kutokukiuka Kanuni za Bunge linalohusika. Kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuathiri masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati zina uwezo wa juu kuhusu utaratibu wa mwenendo wake. Kwa mfano, uwezo wa kuanza kujadili hoja gani kabla ya hoja nyingine na uwezo wa kuamua utaratibu wa kujadili hoja zinazoshughulikiwa na Kamati.

Mamlaka ya kuamua iwapo hoja iliyopelekwa kwenye Kamati ifikishwe Bungeni au laa, si ya Kamati ya Bunge. Sababu yake ni kwamba, jambo hilo halihusu utaratibu. Vilevile, jambo hilo linahusu uwezo au hali ya Bunge kuamuru na kuamua lakini Kamati ni wakala wa Bunge si Bunge lenyewe. Kwa kuwa Kamati ni wakala wa Bunge kuhusu hoja iliyo kwenye Kamati, uwezo wa juu kuhusu hatima ya jambo hilo, (mamlaka) ni wa Bunge lenyewe.

Neno la pili ni 'madaraka'. Kilugha neno hili lina maana uwezo wa kufanya jambo fulani. Uwezo huu unaweza kuwa uwezo uliokasimiwa au uwezo wa asili. Kiistilahi 'madaraka' ya Kamati ya Bunge'



*Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson akizungumza Bungeni*

ni uwezo wa kufanya jambo fulani ndani ya wigo wa majukumu yake. Matokeo ya uwezo huo ni ushauri, maoni au mapendekezo.

Kwa maana hiyo, Kamati inayo madaraka ya kufanyia kazi jambo lililopelekwa mbele yake kwa mujibu wa Kanuni. Kwa mfano, madaraka yanayohusu uchambuzi wa masuala ya matumizi ya fedha za umma na madaraka yanayohusu ufuatiliaji na utekelezaji wa uamuzi wa Bunge kuhusu matumizi ya fedha za umma.

Katika mifano hiyo miwili ya madaraka ya Kamati, matokeo yake ni maoni na mapendekezo ya Kamati kwa Bunge. Angalizo hapa ni kuwa maoni na mapendekezo ya Kamati hayaelekezwi kwa Taasisi, Shirika au Wizara za Serikali kwa kuwa madaraka ya kufanya hivyo ni ya Bunge lenyewe na si ya Kamati ya Bunge. Kamati ikitoa mapendekezo kwa madaraka isiyokuwa nayo, mapendekezo hayo yatakosa msingi na uendeshaji wa aina hiyo hauna mashiko.

Madaraka ya Kamati za Bunge yana matokeo ambayo hutumiwa na Bunge katika mchakato wake wa kujadili hoja hadi kufikia uamuzi. Hii inaopnesha kuwa matokeo ya utekelezaji wa madaraka ya Kamati ni kupatikana kwa msaada wa Kamati kwa Bunge. Kamati zisipotekeleza madaraka yake ipsavyo, Bunge linaweza kupata msaada wa Kamati wenye upungufu au wenye dosari zinazokwamisha uamuzi wa kibunge.

Neno la tatu ni majukumu ambayo ni wingi wa neno jukumu. Kilugha, neno "jukumu" lina maana ya jambo linalomlazimu mtu kulifanya. Kiistilahi, majukumu ya Kamati ya Bunge ni mambo yanayoilazimu Kamati kuyafanya kwa majibu wa Kanuni za Bunge. Kwa mfano kushughulikia maeneo yenye matatizo ya fedha za umma ni jukumu la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Katika mfano huo, inailazimu Kamati ya Bunge kufanya utekelezaji wa mambo yanayogusa maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma. Matokeo ya kutekeleza majukumu ya Kamati ni Ripoti ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Indhari hapo ni kuwa si jukumu la Kamati inayosimamia matumizi ya fedha za umma kuamua iwapo hoja inayohusu matumizi ya fedha za umma inaweza kuingia Bungeni au laa.

Majumuisho ya mambo hayo matatu yanaonesha kuwa Kanuni za Bunge zinabainisha majukumu ya Kamati za Bunge yanayohusu usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Katika kutekeleza majukumu hayo Kamati inao uwezo wa kuamua kufanya au kutofanya mambo kadha wa kadha (madaraka) kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma.

Ili Kamati ya Bunge itumie madaraka yake katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati, inao uwezo wa juu wa kujiongoza kuhusu utaratibu wake. Kwa sababu hiyo, utekelezaji wa madaraka ya Kamati za Bunge huendana na majukumu ya Kamati. Wakati wa kutumia madaraka iliyonayo ili kutekeleza majukumu yake, Kamati inayo mamlaka kamili kuhusu utaratibu wake iwapo itakuwa ndani ya misingi iliyowekwa na Kanuni za Bunge.

Kwa ujumla, inaonekena kwamba, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma ni madaraka ya Bunge lenyewe. Katika utekelezaji wa madaraka hayo, Bunge linategemea karakana yake ya uchambuzi wa kina wa hoja kuhusu matumizi ya fedha za Umma. Karakana hiyo ni Kamati zinazohusika na kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Kamati hizo ni zile zenye madaraka yanayogusa eneo la matumizi mabaya ya fedha za Umma. Madaraka hayo yana matokeo yake kwenye ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma. Matokeo ni Kamati kutekeleza madaraka yake ni Bunge kupata msaada stahiki wa Kamati zinazohusika. Kwa mfano, Bunge linapata mapendekezo ya msimamo wa Kibunge utakaosaidia kupungua kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Kwa madaraka hayo, Kamati inayohusika inapaswa kutekeleza majukumu yake. Yaai inailazimu Kamati kufanya shughuli maalumu zinazowezesha kufanyia kazi mambo yanayohusu matumizi ya fedha za umma kwa kadiri ilivyofafanuliwa kwenye Kanuni za Bunge. Katika hayo, Kamati inayo mamlaka ya juu ya utaratibu wake usiopingana na Kanuni za Bunge.

Kwa kuhitimisha mambo makuu ya kuchukua kuhusu usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma yanahusu mamlaka, madaraka na majukumu ya Kamati. Mawanda ya mambo hayo ni uhusika wa Kamati katika usimamizi wa kibunge wa matumizi ya fedha za umma. Jambo hilo linahitaji mambo matatu.

Jambo la kwanza ni majukumu ya Kamati ambayo matokeo yake ni maoni na mapendekezo kwa Bunge. Majukumu hayo kwa kawaida ni utekelezaji wa madaraka ya Kamati zinazohusika na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Hivyo, utekelezaji huo unaenda pamaja na Kamati kuwa na mamlaka kuhusu utaratibu wake wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati ili kufanikisha utekelezaji bora wa madaraka ya Kamati.

Katika toleo lijalo, safu hii itadadavua mchakato wa kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Bunge la Tanzania. Mahsusi katika toleo lijalo ni namna Kamati za Bunge zinavyolisaidia Bunge kusimamia matumizi ya fedha za umma. Ufafanuzi utazingatia dhana za mamlaka, madaraka na majukumu katika mchakato wa kusimamia matumizi ya fedha za umma.

# Spika wa Comoro atembelea Bunge la Tanzania



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akimkabidhi zawadi Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, Mhe. Moustadroine Abdou.*

*Na. Patson Sobha*

Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, Mhe. Moustadroine Abdou alitembelea Bunge la Tanzania jijini Dodoma wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliofanyika Septemba, 2024.

Mhe. Abdou alifanya ziara ya kwanza ya kikazi ya siku sita nchini jijini Dodoma kuanzia tarehe 31 Agosti, 2024 hadi 5 Septemba, 2024 kufuatia mwaliko wa mwenyeji wake, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Mhe. Dkt. Tulia Ackson.

Akimkaribisha na kumtambulisha Bungeni pamoja na ujumbe wake, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Tulia Ackson, alisema alimwalika Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro kufanya ziara ya kwanza nchini tangu nchi hizi mbili zianzishe uhusiano wa kidiplomasia.

"Waheshimiwa Wabunge, hii ni ziara ya kwanza ya Spika wa Bunge la Visiwa vya Comoro kutembelea Bunge letu tangu nchi zetu mbili zilipoanzisha uhusiano wa kidiplomasia, kwa hiyo tunawakaribisha sana…" alisema Mhe. Spika.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson, aliongeza kusema kwamba "tunawakaribisha wageni wetu, tunaamini kwamba ziara hii itaendelea kukuza ushirikiano kati ya Bunge letu na Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, lakini pia uhusiano kati ya nchi hizi mbili."

Katika ziara hiyo, Mhe. Moustadroine Abdou aliambatana na Naibu Spika wake Mhe. Anfani Hamada Bacar, Mbunge wa Bunge hilo, Mhe. Abdo Rahim Mistoihi, Mkuu wa Sekretarieti ya Bunge, Bw. Soulaimane Abdou Housseine na Mshauri wa Mawasiliano wa Bunge la Comoro Bw. Abdoulwahab Ali Aziri.

Ujumbe wa Spika wa Comoro, uliwasili nchini kwa ndege ya ATC kupitia Kiwanja cha Ndege cha Julius Kambarage Nyerere jijini Dar es Salam na kupokelewa na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Tanzania akiwa ameambatana na Mhe. Vita Kawawa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Maafisa wa Itifaki wa Bunge na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Ujumbe huo ukiambatana na Mhe. Vita Kawawa na kwa madhumuni ya kuona hatua za maendeleo zilizofikiwa na Tanzania, ulianza ziara ya kikazi kwa kusafiri kwa njia ya treni ya mwendo kasi kutoka Dar es salaam hadi Morogoro, ambako ulitembelea Mbuga ya Wanyama ya Mikumi, na kisha

jioni ya siku hiyo kusafiri tena kwa treni kuelekea Dodoma.

Mheshimiwa Abdou, baada ya kutambulishwa ndani ya ukumbi wa Bunge, alitembelea Ukumbi wa Pius Msekwa pamoja na kumbi mbalimbali za Kamati za Bunge zilizopo ghorofa ya tano ya jengo la utawala, na pia kupata maelezo kuhusu picha za viongozi mbalimbali wa Bunge waliopita na waliopo.

Spika wa Comoro na ujumbe wake, walipata pia nafasi ya kutembelea maeneo ya mengine ya Bunge ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya, ambapo pamoja na kupata maelezo ya kituo hicho kinachotoa huduma kwa Wabunge na watumishi wa Bunge.

Ujumbe huo wa Spika wa Bunge la Comoro pia ulipata nafasi ya kutembelea Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kujionea maendeleo ya sekta ya afya nchini Tanzania na kukuza utalii wa kimatibabu kwa wananchi wa Comoro kuja kutibiwa Dodoma.

Katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Mhe. Moustadroine Abdou alikaribishwa na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel, ambaye alimtembeza maeneo mbalimbali ikiwemo sehemu ya huduma ya upasuaji wa moyo, kliniki ya matibabu ya seli mundu pamoja na ujenzi wa jengo jipya la matibabu ya saratani ambalo ni la mfano kwa Afrika.

Akizungumzia maendeleo aliyoyashuhudia na ziara hiyo Spika wa Comoro alisema ameshangazwa kuona Tanzania ina vifaa tiba na watalaam bingwa wanaotoa huduma bora na za kisasa ambazo zamani walitegemea kupata nchi za magharibi, akitolea mfano nchi ya Ufaransa ambako amekuwa akitibiwa.

“Nimeshangazwa sana kwamba huduma hizi bora na za kisasa zinapatikana hapa Tanzania, ambazo siku za nyuma tumekuwa tukipata kwenye nchi za Ulaya, na kwa kweli nathubutu kusema huduma ya meno niliyopata Ufaransa haifikii hii ya Hospitali ya Benjamin Mkapa,” allisema

Pia aliwaasa Watanzania kuthamini kazi kubwa ambayo imefanywa na serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, aliwaasa wamwombee Mheshimiwa Rais ili azidi kuwatumikia Watanzania na kuwasaidia kupata huduma bora za afya kwa ruzuku kama alivyosaidia matibabu ya watoto wenye ugonjwa wa seli mundu.

“Tunashukuru sana kwa yale yote ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia anayafanya siyo tu kwa Watanzania bali hata Wacomoro ambao tunakuja kupata huduma za matibabu hapa Tanzania,” alisema

"Watanzania endeleeni kumwombea ili azidi kuboresha huduma hizi kwa ajili yenu, waafrika na dunia yote waweze kufuata huduma hapa Tanzania” aliongeza Mhe. Abdou.

Akizungumza katika ziara hiyo, Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel, alisema wamepokea ugeni huo kwa heshima kubwa kwa sababu Watanzania na Wacomoro ni ndugu na kuna haja ya kudumisha na kuongeza ushirikiano katika sekta ya afya kwa madaktari wa Tanzania kuwatibu Wacomoro hapa nchini lakini pia kuandaa mpango maalum wa kushirikiano na madaktari wa Comoro kwenda nchini humo kutoa huduma.

Baada ya ziara ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, ujumbe wa Spika wa Comoro ulipewa nafasi ya kufanyiwa uchunguzi wa kiafya na kushauriwa pia kupata nafasi ya kutembelea Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Mloganzila.

Ujumbe huo wa Spika wa Comoro ulihitimisha ziara yake kwa hafla ya chakula cha jioni lichoandaliwa na mwenyeji wake, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Meshimiwa Dkt. Tulia Ackson.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Spika wa Comoro alimpongeza Mhe. Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

“Ninapomwona Mhe. Dkt. Tulia Ackson, namwona ni dada yangu wa damu kabisa! Sisi ni ndugu, na hivyo hatuna budi kudumisha undugu wetu kwa kuongeza ushirikiano wa kibunge kwa kuunda chama rafiki. Pia nampongeza sana Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa kuongoza Umoja wa Mabunge Duniani,” alisema.

Mhe. Abdou alitumia nafasi hiyo kuelezea umuhimu wa kudumisha ushirikiano wa kibunge na kuwa na mpango wa watalaam wa Mabunge hayo mawili kubadilishana uzoefu kwa kuunda vyama rafiki vya kibunge na kutembeleana.

Kwaupandemwingine aliipongeza Tanzania kwa kupitisha sheria mpya ya kuwezesha familia 50 za watanzania wenye asili ya Zanzibar na Comoro kupata uraia wa Tanzania.

Wakibadilishana zawadi katika hafla hiyo, Spika wa Tanzania, alimpa mgeni wake ngao maalum yenye nembo ya Bunge pamoja na mashuka mawili ya kimasai, moja kwa ajili yake na lingine kwa mwenzi wake.

Aidha, Mhe. Dkt. Tulia alimkirimu pia mgeni huyo korosho, kahawa, na majani ya chai vyote vinavyozalishwa hapa nchini.

Kwa upande wa Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, yeye alitoa zawadi ya sanamu maalumu ya ramani ya muungano wa visiwa vinne vikuu vya Comoro kikiwepo Mayotte, Anjouan, Moheli, na Ngazidja.

Aidha, alitoa zawadi ya kanga ambayo alisema ni vazi rasmi kwa wananchi wa visiwa hivyo.

Baada ya kuhitimisha ziara yake, Mhe. Abdou, ambaye pamoja na kuwa Spika wa Bunge la Muungano wa Visiwa vya Comoro, amewahi kuwa Rais wa Mpito na Makamu wa Rais wa nchi hiyo, aliondoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa treni ya SGR na kisha kurejea nchini kwake salama.

# Kamati: Sheria zilinde Maslahi ya Nchi

*Na. Halima Laizer*

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imebaini dosari katika uchambuzi wa Sheria Ndogo 38 na Maazimio 22 ya Sheria Ndogo.

Kamati hiyo iliainisha dosari hizo wakati ikiwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu uchambuzi wa Sheria hizo pamoja na maazimio ya Kamati katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge uliofanyika tarehe 27 Agosti hadi tarehe 6 Septemba, 2024.

Akiwasilisha taarifa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza alisema Kamati ilibaini dosari mbalimbali katika Sheria hizo.

Alizitaja dosari hizo kuwa ni pamoja na kukinzana na masharti ya Katiba na kwamba nia ya Sheria Ndogo ni kufanikisha lengo kuu la sheria mama inayotungwa na Bunge na sio kukinzana na Katiba.

"Sheria Ndogo kama zilivyo sheria nyingine za nchi zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni msingi mkuu wa sheria za nchi zikiwemo sheria mama.

"Hata hivyo, uchambuzi unabainisha baadhi ya Sheria Ndogo zenye maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba," alisema.

Mheshimiwa Dkt. Rweikiza alisema, Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake na kwa kuwa dosari hizo zinaathiri tija ya sheria mama na kuruhusu utungwaji wa Sheria Ndogo na zinaweka ugumu katika usomaji wa sheria mama kwa pamoja na ufafanuzi wa Sheria Ndogo.

"Dosari hizo zinazuia utekelezaji wa sheria mama kutokana na kutofafanuliwa ipasavyo au kutoendana na dhamira ya sheria mama na sheria nyingine za nchi," alisema.

Alisema mamlaka zinazotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zirekebishe dosari za Sheria Ndogo zinazozohusika.

Akichangia taarifa hiyo, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan alisema Serikali imekuwa ikifanya maboresho kwenye Sheria Ndogo nyingi na kwamba Sheria Ndogo moja inaweza kuwa na makosa zaidi ya 10 hadi 20.

Alimpongeza Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara kwa ujumla wamekuwa wakizipeleka Sheria Ndogo za Halmashauri za Mamlaka ya Miji, Wilaya na Vijiji kwenye Kamati ya Sheria Ndogo ili izipitie na kuzipitisha kabla ya kutangazwa kuwa sheria.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza akiwasilishaTaarifa ya Kamati Bungeni*

Akichangia taarifa hiyo, Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho alishauri maboresho zaidi katika uwasilishwaji wa Sheria Ndogo katika Kamati.

Kwa upande wake Mheshimiwa Benaya Kapinga alishauri Halmashauri husika inayohusika na kutunga Sheria Ndogo kufika kwenye Kamati ili kutoa ufafanuzi badala ya Waziri peke yake.

Mheshimiwa Abdallah Chikota alishauri baadhi ya Halmashauri kukusanya ushuru muda wowote ule badala ya kujiwekea muda maalum katika sheria zao.

Akijibu baadhi ya hoja hizo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Johari alisema, idadi ya Sheria Ndogo zinazokinzana na masharti ya Katiba zimepungua.

"Dalili ni nzuri, tukiongeza bidii katika kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Kamati, idadi ya Sheria Ndogo zinazokinzana na masharti ya Katiba zinaweza kupungua kabisa na kuwa sifuri," alisema.

Mheshimiwa Johari alisema mojawapo ya hatua zinazochukuliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kutengeneza mwongozo kwa Mawakili wote wa Serikali nchini ili uweze kusaidia katika utengenezwaji wa sheria ndogo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mheshimiwa William Lukuvi alisema Serikali imepokea mapendekezo ya Kamati na watafanyia kazi.

Aidha, alizitaka mamlaka zote katika uandishi wa sheria zao kuwa ni lazima wamshirikishe Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Na katika hili, Serikali hailali na itahakikisha kwamba jambo hili linaratibiwa na Sheria Ndogo zitakazo kuwa zinatangazwa lazima zikidhi malengo na matarajio ya wananchi," alisema.

Katiba inalipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na kwa mantiki hiyo utungaji wa sheria zote upo kwenye mamlaka ya Bunge.

Kamati ya Sheria Ndogo imepewa majukumu na mamlaka ya kukaa na kupitia Sheria Ndogo zote kwa niaba ya Bunge.

# Dkt. Ndugulile Achaguliwa WHO

Na.Deoniusius Simba

MBUNGE wa Jimbo la Kigamboni, Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile amechaguliwa kushika wadhifa wa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa Ukanda wa Afrika ambapo ataongoza nchi 47.

Nyota ya Dkt Ndugulile ilianza kung'ara baada ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuidhinisha jina lake kwenda kugombea nafasi hiyo ambayo kabla ilikuwa ikishikiliwa na Dkt. Matshidiso Moeti kutoka Botswana.

Mbunge huyo wa Kigamboni aliingia kwenye kinyang'anyiro hicho na kuwashinda wagombea wengine

Mkutano huo wa 74 wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika uliofanyika nchini Congo katika mji wa Brazzaville na baada ya marudio ya kura Dkt. Ndugulile akapata jumla ya kura 25 akifuatiwa na mgombea kutoka Senegal aliyepata kura 14 wakati mgombea kutoka Niger akipata kura sita.

Mkutano huo ulifunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Congo Brazaville, Mhe. Denis Sassou Nguesso huku kukiwa na ushindani mkali kutoka kwa wagombea kwa namna nchi zilivyokuwa zimejipanga.

katika nafasi ya Naibu Waziri wa Afya katika Serikali ya Awamu ya Tano, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya ushauri ya Masuala ya Afya ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) katika uchaguzi uliofanyika Jijini Luanda nchini Angola.

Taratibu katika nafasi hizo zinamtaka mteule kuthibitishwa na Kikao cha Bodi ya Utendaji ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ambacho kwa sasa kinatarajia kukaa mwezi Februari 2025 huko Geneva nchini Uswisi.

Marakikao hicho kitakapomthibitisha,



*Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akimpongeza Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika.*

ambao ni; Dkt. Boureima Hama Sambo (Niger); Dkt. N'da konan Michael Yao (Cote d'Ivoire); Dkt. Ibrahim Soc'e Fall (Senegal) na Dkt. Richard Mihigo (Rwanda).

Mawaziri wa Afya katika nchi za Ukanda wa Afrika ndiyo walikuwa wapiga kura kwenye uchaguzi huo uliofanyika Agosti 27, 2024 huku jumla ya nchi 19 zilipiga kura kwa Tanzania, 12 zikiipa Senegal na nchi za Rwanda na Niger kila moja ilipata kura saba.

Safari ya Dkt. Ndugulile ilianzia Machi 11, 2023 baada ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Afya ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Nafasi hiyo ilipelekea kuwa miongoni mwa Wabunge 12 wanaoishauri IPU kuhusu masuala ya afya duniani nafasi ambayo alipaswa kuitumikia kwa kipindi cha miaka minne.

Oktoba 24, 2023 Mbunge huyo ambaye amewahi kuhudumu

itamlazimu Dkt. Ndugulile kujiuzulu nafasi yake ya Ubunge na hivyo jimbo hilo kubaki wazi.

Hata hivyo kwa mujibu wa sheria za uchaguzi Tanzania, wananchi wa Kigamboni hawatakuwa na uchaguzi mdogo wa jimbo kwani muda anaojiuzuru na ule utakaobaki katika uhai wa Bunge la 12 hautaruhusu kufanyika kwa uchaguzi mdogo badala yake watasubiri uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka 2025.



Hayati Chifu Adam Sapi Mkwawa enzi za uhai wake akiwa Spika wa Bunge

# Kutoka Chifu hadi Spika wa Bunge

Na. Patson Sobha

Ngome ya Kalenga, iliyopo Wilaya ya Iringa Vijijini, mkoani Iringa, ina historia kubwa ya kipekee, baada ya ile ya Mkwavinyika Munyigumba Mwamuyinga, almaarufu Chifu Mkwawa, kuwapiga na kuwasumbua sana Wajerumani. Safari hii historia inaandikwa kwa mjukuu wake Chifu Adam Sapi Mkwawa kuwa Spika pekee aliyekalia kiti cha uongozi wa Bunge kwa miongo mitatu.

Historia hii inaweza kudumu kwa miaka mingi ijayo na hasa baada ya Maspika wote waliofuata baada ya Chifu Mkwawa kumaliza uongozi wao kwa awamu moja au mbili tu, lakini kwa kuwa hakuna sheria wala kanuni inayozuia uongozi wa Spika kuendelea kwa awamu nyingi, basi pengine tuwe na subira, kama wahenga walivyosema kwamba subira yavuta heri. Heri hii yaweza kuwa kwa Spika aliyepo sasa ama yeyote atakayekuja miaka mingi ijayo.

**Nafasi ya Spika**

Bunge la Tanzania na kabla ya hapo kwa upande wa Tanganyika liikitwa Bunge la Tanganyika, limewahi kuongozwa na Maspika mbalimbali kuanzia mwaka 1953 kufuatia Baraza la Kutunga Sheria *(LegCo)* kubadilisha utawala wake kutoka kwa Gavana wa Tanganyika aliyekuwa pia ndiye Rais (Mwenyekiti) wa Baraza na sasa kuwa na kiongozi aliyejulikana kama Spika kwa mara ya kwanza.

Kumekuwa na maelezo mengi na hata wanafunzi wa shule za msingi wamekuwa wakifundishwa kuwa Spika wa Kwanza wa Bunge katika historia ya Tanzania ni Chifu Adam Sapi Mkwawa. Wanaosema hivyo, watakuwa sahihi ikiwa tu wanamaanisha wa kwanza mwenye asili ya Afrika ama wa kwanza kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, aliyeitwa Spika wa kwanza kuongoza muhimili wa Bunge alikuwa Brigedia Sir. William Erick Halstead Scupham aliyeteuliwa na Malkia wa Uingereza tarehe 1 Novemba, 1953.

Brigedia Sculphum aliongoza Baraza la Kutunga Sheria kwa miaka mitano hadi tarehe 30 Aprili, 1958 alipochaguliwa Spika

wa pili Sir. John Harry Barclay Nihill ambaye alianza kazi ya spika tarehe 1 Mei, 1958 hadi 31 Desemba, 1959 alipofariki dunia akiwa nchini Uingereza. Wajumbe wa Bazara walimchagua aliyekuwa Naibu Spika, Bw. Abdulkarim Yusufali Alibhai Karimjee.

Karimjee aliyekuwa raia wa Uingereza mwenye asili ya Asia, alitumikia nafasi ya Spika kwa miaka mitatu wakati Tanganyika iko katika harakati za kupata uhuru na hatimaye kuwa Jamhuri mwaka 1962, ambapo Wabunge walimchagua Chifu Adam Sapi Mkwawa kuwa Spika wa Bunge na Naibu Spika wake akiwa Chifu Erasto Mang'enya (Chifu wa Wabondei).

Chifu Adam Sapi alikuwa Spika wa Bunge kuanzia mwaka 1962 hadi 1973 pale alipoteuliwa na Rais, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuwa Waziri wa Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, ambapo Wabunge walimchagua aliyekuwa Naibu Spika wake Chifu Erasto Mang'enya kuwa Spika wa Bunge mwaka 1973 hadi 1975.



Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 1975, Chifu Mkwawa akarejea kugombea nafasi ya Spika na Wabunge wakamchagua kwa mara nyingine, ambapo aliendelea kuwa Spika kwa vipindi vyote vya Bunge vilivyofuata hadi mwaka 1994 alipoamua kujiuzulu kwa hiari yake mwenyewe kutokana na hali ya uzee na afya kutetereka, kisha aliyekuwa Naibu wake, Mhe. Pius Msekwa akachaguliwa kuwa Spika.

**Kuzaliwa kwake**

Chifu Adam Sapi, alizaliwa tarehe 16 Juni, 1920 katika familia ya Utawala wa Kabila la Wahehe kwenye Ngome ya Kalenga, Iringa, alipata elimu yake ya sekondari katika Shule ya Tabora na baadaye kujiunga na Chuo Kikuu cha Makerere, ambako kutokea huko aliitwa kurudi nyumbani ili atawazwe kuwa Chifu akimrithi baba yake Chifu Sapi Mkwawa ambaye naye alichukua utawala kutoka kwa Chifu Mkwavinyika Munyigumba Mwamuyingaa (Mkwava) aliyepambana na kuwasumbua sana Wajerumani.

**Rekodi ya Pekee**

Pamoja na kwamba Maspika wote waliowahi kuongoza Bunge na hata Dkt. Tulia Ackson anayeongoza kwa sasa, wamefanya mengi na makubwa ya kukumbukwa na yenye rekodi za aina yake, lakini hili la Chifu Adam Sapi Mkwawa kukalia Kiti cha Spika kwa jumla ya miaka 30, halina mfano wake.

Ukiacha rekodi hiyo ya miaka 30, kuna zingine ambazo Chifu Adam Sapi aliweka ikiwemo kuteuliwa kuwa miongoni mwa Wajumbe wa mwanzo kabisa wenye asili ya Tanganyika kuingia kwenye Baraza la Kutunga Sheria la Tanganyika. Mkwawa aliteuliwa na Gavana wa Tanganyika na kuapishwa ndani ya Baraza tarehe 3 Juni, 1947 akiwa mjumbe wa tatu baada ya machifu wawili kuteuliwa kabla yake.

Itakumbukwa kuwa tangu kuundwa kwa Baraza la Kutunga Sheria mwaka 1926, hakukuwa na Wajumbe wenye asili ya Tanganyika hadi karibu miaka 20 baadaye ambapo tarehe 24 Novemba, 1945 waliteuliwa Chifu Kidaha Makwaia kutoka Shinyanga na Chifu Abdieli Shangali kutoka Kilimanjaro, ambao uteuzi wao uliwekwa kwenye Tangazo la Serikali Namba 1046 la tarehe 30 Novemba.Baadaye wakafuatiwa

na Chifu Adam Sapi na wa nne alikuwa Bw. Juma Mwindadi aliyeteuliwa tarehe 1 Aprili, 1948.

Chifu Adam Sapi aliweka rekodi nyingine ya kuwa miongoni mwa Waafrika (Watanganyika) wa kwanza kuwa Wajumbe wa Baraza la Kumshauri Gavana. Gavana alimteua Chifu Kidaha Makwaia tarehe 16 Aprili, 1951 na kisha Chifu Adam Sapi Mkwawa akateuliwa tarehe 25 Mei, 1954.

**Kuingia kwenye siasa**

Kwa upande wa siasa, Chifu Mkwawa alikuwa miongoni mwa Machifu wachache wa kwanza waliounga mkono Chama cha TANU na juhudi za kupigania uhuru. Ilikuwa mwaka 1955 pale Bw. Abdulwahid Sykes na Bw. Dosa Aziz walipoalikwa kwenye shughuli ya kupokea fuvu la Kichwa cha Babu yake, Chifu Mkwavinyika Munyigumba Mwamuyinga, walimwingiza kwenye uanachama wa TANU kwa siri.

**Kapteni wa Jeshi**

Chifu Adam Sapi Mkwawa, alikuwa Mwafrika wa kwanza nchini kupewa Cheo cha Heshima cha Kapteni wa Jeshi la Wakoloni wa Uingereza la *King's African Rifles (KAR)*. Aidha, Mtwa Adam Sapi, alishikilia rekodi ya kuwa Mbunge aliyekaa Bungeni kwa miaka mingi kuliko Mbunge mwingine yeyote. Alikuwa Mbunge kwa kipindi cha miaka 47 kuanzia mwaka 1947 hadi 1994.

**Waziri wa CDA**

Katika kipindi cha mwaka 1973 hadi 1975 aliteuliwa kuwa Waziri wa Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Hii ni rekodi nyingine kwa kuwa Wizara hii ilianzishwa maalum kama sehemu za jitihada za kuendeleza Mji wa Dodoma ili kuwa Makao Makuu ya nchi na ya Utawala wa Serikali. Katika juhudi hizo, Bunge liliunga mkono na kuhamishia baadhi ya mikutano yake mifupi kuanza kufanyika Dodoma katika Ukumbi wa CCM Makao Makuu.

Kukaa kwa miaka 30 katika Kiti cha Uongozi wa Bunge haikuwa bure kwa Chifu Mkwawa, kwani mambo makubwa yalifanyika wakati wa uongozi wake ikiwemo mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika, Katiba ya Mpito na Katiba ya Kudumu ya mwaka 1977. Aidha, katika kudumisha Muungano, Bunge likiongozwa na Spika Mkwawa, lilifanyaa Mkutano wake wa Bajeti katika Kisiwa cha Unguja mwaka 1977 na pia Kisiwa cha Pemba mwaka 1978.

**Vazi la Spika**

Jambo lingine la kipekee kabisa ambalo Chifu Adam Sapi Mkwawa alilifanya ni kubadili utaratibu wa Spika kuvaa Joho Jeusi na wigi la nywele nyeupe za kizungu kama wanavyovaa majaji. Mkwawa aliamua kuvaa vazi la kichifu la kanzu huku akijifunika shuka na kilemba. Baadaye akabadili na kuanza kuvaa kanzu nyeupe na kujizungushia kanga maalum yenye nakshi za mazao ya biashara na alama za utamaduni wa Mtanzania, vazi ambalo likaboreshwa zaidi na Kamati iliyoundwa kubuni vazi hilo baada ya Mhe. Pius Msekwa aliyekuwa Spika kutokuwa na asili ya uchifu kama ilivyokuwa kwa Chifu Mang'enya na Chifu Mkwawa. Vazi lililobuniwa wakati wa uongozi wa Pius Msekwa, ndilo joho maalum linalotumiwa hadi sasa.

**Kujiuzulu**

Chifu Adam Sapi Mkwawa, anakumbukwa pia kwa kuwa Spika wa kwanza kuamua kwa hiari yake mwenyewe kujiuzulu. Ilikuwa amalize kipindi chake cha uongozi wa Bunge mwaka 1995, hata hivyo mwaka 1994 aliamua kutoa Taarifa ya Spika kwa Wabunge na kuwajulisha kwamba anajiuzulu kutokana na sababu za uzee na afya kuanza kutetereka.

Baada ya kuwatumikia Watanzania kwa miongo mitatu akiwa Spika na jumla ya miaka 47 akiwa Mbunge, huku Taifa likishuhudia mabadiliko makubwa ya sheria zilizopitishwa Bungeni chini ya uongozi wake, wakati wa mfumo wa vyama vingi na baadaye chama kimoja, kisha kurejea kwa vyama vingi mwaka 1992, Chifu Mtwa Adam Sapi Mkwawa, Mjukuu wa Mkwavinyika Munyigumba Mwamunyinga, aliaga dunia tarehe 25 Juni, 1999.

Chifu Mkwawa alirithiwa na mtoto wake Chifu Abdul Adam Sapi Mkwawa, ambaye alifariki mwezi Februari, 2015 na akatawazwa mtoto wake Adam Abdul Adam Sapi Mkwawa na kuchukua jina la Mfwimi wa II. Hata hivyo kwa kuwa Mfwimi II alikuwa bado mdogo wa umri wa miaka 14, ilibidi Baba yake Mdogo Hassan Mkwawa achukue madaraka kwa muda hadi Adam atapofikisha umri wa miaka 20. Kwa hivi sasa Chifu Adam Abdul Adam Sapi Mkwawa (Mfwimi II) amesimikwa rasmi kwa kuwa ana umri wa miaka 23.

# Umuhimu wa Kamati za Bunge Katika

Na. Athuman Hussein, ndc
a.brambat@bunge.go.tz

Umuhimu wa Kamati za Bunge katika utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Bunge ni makala inayoendelea kutoka toleo la saba. Toleo hilo lilimalizia kwa kunasihi kwamba "***Elimu ni mali, Adui hawezi kukunyang'anya***".

Kinachokusudiwa ni kuwa, uelewa alioupata mtu kuhusu umuhimu wa Kamati za Bunge, unabaki kwa mwelewa. Hakuna awezaye kuupora. Kwa maana hiyo aliyebaki na uelewa huo katika toleo lililopita, basi kaelewa hata kama atatokea asiyependa mhusika awe na uelewa. Wito tuendelee na mfululizo wa makala hii. Wito huu unakubaliana na busara kwamba, "***Aliyepeleka mkono, kutamalaki si kazi***."

Maelezo hayo yanakusisitiza msomaji wa Makala hii uendelee kujikusuru kufuatilia maudhui muhimu juu ya Kamati za Bunge. Kufanya sahala ya usomaji, huenda ikafaa kukumbusha baadhi ya mambo muhimu katika toleo lililopita.

Toleo la saba pamoja na mambo mengine, lilionesha kwamba, Kamati ya Bunge ni chombo kikuu kinachoimarisha utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Bunge. Kudorora kwa uendeshaji wa Kamati za Bunge ni jambo linaloweza kuathiri ***natija*** ya Bunge.

Lingine lililofafanuliwa ni kuhusu mfumo na ufanisi wa Kamati za Bunge kuwa kiini cha uhakiki na tathmini ya ufanisi wa Bunge. Hawezi mfuatiliaji au mchambuzi wa masuala ya Bunge kuelezea uendeshaji wa Bunge kwa ufanisi au kujadili vizuri utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Bunge iwapo, hana uelewa unaofaa kuhusu Kamati za Bunge na mfumo wake.

Aidha, ilibainisha kuwa desturi ya Bunge kuchakata hoja inategemea kwa kiasi kikubwa matokeo ya kazi za Kamati. Msisitizo kwa hilo ni kuwa, ubora wa mchakato wa hoja Bungeni na matokeo yake, haupatikani iwapo kazi za Kamati za Bunge zitakosa umakini, kina stahiki na tija. Ndio maana ikasemwa Kamati za Bunge ni injini ya Bunge. Hakuna uendeshaji wa Bunge bila Kamati kama ilivyo hakuna gari linalotembea bila injini.

Vilevile, katika Toleo lililopita, ilidokezwa kwamba, dhana ya Kamati za Bunge inawakanganya wadau wengi wa masuala ya Bunge. Ushahidi wa mtazamo huo ulikuwa ni chapisho la waandishi wa masuala ya kibunge, Kyle na Peacy (2002). Kwa msingi wa maelezo yote hayo, yeyote anayetoa maoni kuhusu kazi, uendeshaji au ufanisi wa Bunge, atakosa msingi iwapo hatakuwa na uelewa mzuri kuhusu Kamati za Bunge.

Mhakiki, mchambuzi au mtafiti yeyote asiyekuwa na uelewa kuhusu Kamati za Bunge, ataweza kulaumu au kupongeza, kusifia au kushutumu, lakini bila mashiko ya mtazamo wake. Ingelikuwa ni daktari, ingelisemwa kwamba, mtu huyo ataweza kueleza dawa anayoweza kutumia mgonjwa bila taaluma. Madhara ya maoni kuhusu ufanisi wa Bunge bila uelewa kuhusu Kamati hayatofautiani kwa kiasi kikubwa na madhara ya asiye na elimu ya utabibu kufafanua dozi ya dawa kwa mgonjwa.

Kwa uelewa huo, makala ilianza na maana ya Kamati za Bunge. Mwanzo wa fasili ulikuwa ni waandishi Johnson na Nakumara walioandika kitabu cha kuwapa Wabunge wapya maelezo ya awali ya kazi yao. Mwingine ni mwandishi Kaare aliyeandika kuhusu Kamati za Bunge katika Demokrasia ya Ulaya. Maelezo ya waandishi hao yanajumuishwa kwa kueleza kuwa, Kamati za Bunge ni Wabunge walio katika mfumo wa Bunge linalohusika.

Katika toleo hili, mwendelezo wa umuhimu wa Kamati za Bunge unajitokeza kwa kufanya mapitio ya Kanuni za Bunge la Tanzania ili kubaini vipambanuzi vitano vilivyotajwa kwenye toleo lililopita. Vipambanuzi hivyo ni: Kamati kutofautiana na Bunge kimuundo, Kamati ni baadhi ya Wabunge au Wabunge katika utaratibu tofauti na Bunge na kuwa Kamati ni kitovu cha Bunge.

Aidha, Kamati kutokuwa na uamuzi kamili wa hoja iingiayo Bungeni na lingine ni Kamati kuwa na uhuru kuhusu utaratibu wa kujiendesha. Lingine litakuwa ni kuhitimishwa kwa kazi za Kamati Bungeni na kuanza kwa mjadala wa Bunge kutoka hitimisho la Kamati. Muhimu katika yote hayo, itaoneshwa uhusiano wa kiuwakala na kiuwakilishi kati ya Kamati za Bunge na Bunge lenyewe.

Kwa kuanzia, **suala la kwanza** ni Kamati kutofautiana na Bunge kimuundo, Kanuni za Bunge zinafafanua na kuweka bayana. Ili kulipata vizuri jambo hilo, ni muhimu kutambua aina kuu mbili za Kamati kwa namna Kanuni zinavyofafanua. Katika ufafanuzi, Kanuni za Bunge zimetungwa na Bunge lenyewe chini ya Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge lenyewe limetokana na masharti

# a Utekelezaji wa Majukumu ya Bunge

ya Katiba.

Kamati za Bunge zimeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge tofauti na Bunge linaloundwa kwa masharti ya Katiba. Bunge limeruhusiwa kuwa na Kamati zake kwa ajili ya utekelezaji bora wa madaraka yake. Kwa msingi huo Bunge lina Kamati zilizoundwa na baadhi ya Wabunge na Kamati ambazo ni sehemu ya hatua ya Bunge kwenye Kikao cha Wabunge wote. Aina ya kwanza ndiyo hasa inayofafanuliwa.

Kwa mtiririko huu mapitio ya Kanuni za Bunge yanafanyika kwa kujikita kwenye Kamati ambazo kwa asili, wajumbe wake si Wabunge wote bali ni baadhi yao. Hapa, zipo Kamati za Kudumu za Bunge, Kamati Maalumu, Kamati Teule na Kamati ya Pamoja. Kamati Maalumu, Kamati Teule na Kamati ya pamoja huundwa kwa jambo maalumu na kuisha muda wake baada ya kutimiza utekelezaji wa jambo hilo tofauti na Kamati za Kudumu.

Kamati za Kudumu zimeanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 137 ya Kanuni za Bunge ambayo imeelekeza kuwa, muundo na majukumu ya Kamati ufafanuliwe kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kamati hizi zina Wajumbe ambao ni baadhi wa Wabunge si Wabunge wote. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri au Naibu Waziri.

Wabunge hao hawawezi kuteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati yoyote ya Kudumu ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 135 (1) ya Kanuni za Bunge. Wabunge wengine hawawezi kuwa wajumbe wa kawaida wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa wakati mmoja.

Kanuni ya 135 (3) ya Kanuni za Bunge inaweka bayana kwamba kila Mbunge atawekwa kwenye kamati mojawapo na si kwenye Kamati zote. Maana yake ni kuwa, Mbunge anaweza kuwa mjumbe wa Kamati fulani na si mjumbe wa Kamati nyingine. Kwa maelezo hayo, Kamati moja inaundwa na baadhi tu ya Wajumbe kama ilivyobainishwa katika vipambanuzi vilivyoelezwa vya kutofautisha Bunge na Kamati zake. Hivyo, Wahakiki, Wachambuzi na Wadau wengine wasijikanganye kwenye maoni yao kuhusu Bunge au kuhusu Kamati za Bunge.

**Suala la pili** ni kuhusu Kamati za Bunge kuwa kitovu cha Bunge. Neno kitovu lina maana mbalimbali katika lugha ya kiswahili. Mojawapo ya tafsiri inachukulia kuwa, kitovu ni mwanzo wa jambo fulani kwa maana hiyo Kamati za Bunge ni mwanzo wa hoja za Bunge.

Vilevile, kitovu ni sehemu maalumu pa kupatia ufumbuzi wa jambo fulani. Hii inaonesha kuwa Kamati ni mahali pa kupatia undani wa jambo linalofanyiwa kazi na Bunge. kwa maneno mengine, Kamati za Bunge ni kituo kikuu cha uchambuzi wa hoja zinazofanyiwa kazi za Bunge. Kwa kawaida mwelekeo wa uamuzi wa Bunge unazaliwa kwenye Kamati ya Bunge kabla ya kufika kwenye Bunge lenyewe.

Kanuni za Bunge zimetambua kituo kikuu cha hoja kwa kuweka sharti la jumla kuhusu hoja kuu zitakazofanyiwa kazi na Bunge. Kanuni ya 60 ya Kanuni za Bunge inaonesha masharti ya mjadala wa mambo yanayoingia Bungeni. Katika masharti hayo, Kanuni ya 60 (3) ya Kanuni za Bunge inaonesha kuwa hoja kuu inayojadiliwa na Bunge sharti ianzie kwenye Kamati ya Bunge.

Kwa msisitizo huo, Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Bunge inaonesha mambo makuu matatu kuhusu nafasi ya Kamati kwenye hoja inayoingia Bungeni. **Kwanza**, si Kamati zote zinapelekewa hoja, bali ni Kamati inayohusika tu ndiyo inayopelekewa hoja. **Pili**, Kamati inayohusika itapaswa kuifanyia kazi hoja iliyopelekwa kwake mapema iwezekanavyo.

**Tatu**, chini ya Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Bunge ni zuio la jumla kuhusu hoja kuu iliyopelekwa kwenye Kamati kutolewa Bungeni kabla ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayohusika kutoa taarifa. Kanuni hiyo inataka hoja itolewe Bungeni baada ya Mwenyekiti wa Kamati kumtaarifu Spika kwamba, Kamatiimemaliza kufanyia kazi hoja.

Masharti hayo yanabeba dhana ya Kamati kuwa kitovu cha hoja kuu itakayojadiliwa na Bunge. Kamati ndiyo inayoijadili kwa kina hoja hiyo na inapewa muda mrefu wa kujadili kuliko Bunge. Inapokuwa na ugumu inapewa muda wa kutosha. Ndio maana kuna katazo la jumla la kutoa hoja Bungeni kabla ya Mwenyekiti wa Kamati inayohusika kutoa taarifa ya kukamilisha kazi.

**Suala la tatu** ni kuhusu Kamati kuhitimisha kazi yake kwenye Kikao cha Bunge. Kwa kawaida Kamati ni nyenzo ya Bunge katika kufanyia kazi hoja kabla ya uamuzi. Kanuni ya 60 (6) ya Kanuni za Bunge inaweka utaratibu kwamba, mara baada ya kutoa hoja kuwasilisha Bungeni hoja yake (Hoja Kuu), Mwenyekiti wa Kamati aliyofanyia kazi hoja

hiyo atatoa maoni ya Kamati.

Ufafanuzi wa utaratibu huo ni kuwa, Bunge litaanza kushughulikia hoja katika hatua ya Kikao cha Bunge kwa kumsikiliza mtoa hoja. Baada ya mtoa hoja, Kamati itawasilisha matokeo ya kazi yake ya uchambuzi ikiwa ni maoni yake. Hii inadhihirisha kuwa, mwisho wa kazi ya Kamati si kwenye Kamati bali inafika kwenye Kikao cha Bunge.

Kanuni ya 60 (7) ya Kanuni za Bunge inabainisha kwamba, baada ya mjadala kumalizika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi wa Bunge. Kwa masharti hayo, hoja itakuwa imefikia mwisho na kazi ya Kamati kushughulikia hoja hiyo itakuwa imefika tamati. Ndio kusema kuwa, kazi ya Kamati kushughulikia hoja itatamatika kwenye Kikao cha Bunge ambacho kitamalizia kwa kufanya uamuzi.

Iwapo, ni hoja ya Kamati iliyoijadili, utaratibu unahusisha Kamati kuwasilisha hoja na uamuzi kufanywa na Bunge lenyewe. Masharti ya utaratibu huo yamefafanuliwa kwenye Kanuni ya Bunge.

Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni ya Bunge, imeweka masharti kwamba, kila Kamati ya Kudumu ya Bunge italazimika kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake. Taarifa hizo zinawasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Ufafanuzi wake ni kuwa, kwa kipindi cha mwaka mzima Kamati zilifuatilia utekelezaji wa shughuli za umma na kutathimini hali ilivyo. Matokeo ya kazi hizo za Kamati hukamilika kwa kuwasilishwa Bungeni. Bunge linapojadili taarifa ya Kamati hutumia utaratibu wa hoja ambapo, taarifa za aina hiyo hujukikana kama hoja za Kamati. Hivyo, hatima yake ni uamuzi wa Bunge.

Kwa ufafanuzi zaidi, Kamati ya Bunge inaweza kuwasilisha muswada wa sheria ambao ni muswada binafsi wa Sheria. Bado utaratibu ni uleule kwamba, shughuli ya kuandaa muswada kwenye Kamati ya Bunge haishii kwenye Kamati. Hatima ya



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba

shughuli hiyo nayo ni kwenye Kikao cha Bunge.

**Suala la nne**, Kamati kutokuwa na uamuzi kamili kuhusu hoja iingiayo Bungeni. Uwezo wa Kamati ni kutoa maoni yake Bungeni na siyo kuamua kuibadilisha au kuirekebisha hoja au muswada. Kwa maneno mengine, uamuzi wa marekebisho yoyote kuhusu hoja si mamlaka ya Kamati.

Kanuni ya 60 (5) ya Kanuni za Bunge imeonesha masharti kuhusu uwezo wa Kamati iliyopelekewa hoja kufanya marekebisho au mabadiliko ya hoja hiyo. Masharti hayo yanaitaka Kamati inayoona kuwa mabadiliko au marekebisho ya hoja yanahitajika, ishauriane na mtoa hoja. Masharti haya ynaonesha kuwa Kamati haina mamlaka kamili kuhusu hopja va vijenzi vya hoja.

Vilevile kwa upande wa Kamati inayoshughulikia Muswada wa sheria haiwezi kurekebisha muswada ila kwa kushauria na Waziri au Mbunge anayehusika.

Hivyo, katika utungaji wa sheria hali kadhalika, Kamati haina uamuzi kamili. Ikiona inafaa itapaswa kushauriana na Waziri au Mbunge anayehusika.

**Suala la tano**, linahusu uhuru wa Kamati katika utaratibu wa kujiendesha. Uhuru huu ulielezwa kuwa jambo la msingi kwa ufanisi wa Kamati. Mantiki yake ni muhimu ili kuwezesha ufanisi, katika uchunguzi, uchambuzi




na Sheria, katika moja ya vikao Kazi, Jijini Dodoma

na uchanganuzi wa masuala ndani ya wigo wa majukumu ya Kamati. Kwa ujumla, uhuru wa kiutaratibu katika Kamati za Bunge unafanikisha usimamizi wa haki, uamuzi sahihi, uwajibikaji na uwazi pamoja na mawazo tofauti.

Kwa umuhimu huo, Kanuni ya 136(8) ya Kanuni za Bunge imezipa Kamati za Kudumu za Bunge, uhuru wa kiutaratibu. Hata hivyo, uhuru huo umewekewa mipaka kwamba, usikinzane na masharti ya jumla ya Kanuni za Bunge. Mipaka ya uhuru huo imewekwa ili kuhakikisha kuwa kuna uthabiti wa masharti ya Kanuni za Bunge hususan kuhusu utaratibu. Vilevile, uhuru huo unahitaji kudhibitiwa kwa uangalizi na uhakika wa Kamati kutokuzidi mamlaka yake.

Mambo hayo matano yanahitaji kueleweka sanjari na yaliyotangulia. Kifupi na kwa ujumla, toleo hili limefanya rejea kwa kuonesha mambo kadhaa. **Kwanza**, Kamati ni chombo kikuu cha kuimarisha utekelezaji wa majukumu na madaraka ya Bunge. **Pili**, desturi ya Bunge kuchakata hoja inategemea kwa kiasi kikubwa matokeo ya kazi za Kamati. **Tatu**, dhana ya Kamati imekuwa ikiwakanganya baadhi ya wachambuzi, wahakiki, watafiti na wadau wengine wa masuala ya kibunge. Hatari yake ni kwenye maoni wanayoyatoa kuhusu Bunge.

Mambo mengine matano yaliyobainishwa kwa kurejea Kanuni za Bunge ni **kwanza**, Kamati za Bunge kuwa kitovu cha ufanisi wa Bunge. **Pili**, Wajumbe wa Kamati kuwa ni baadhi tu wa Wabunge na si Wabunge wote.

**Tatu**, kazi za Kamati kuishia kwenye vikao vya Bunge badala ya kuwa uamuzi kamili na kwamba linaishia kwenye vikao vya Bunge kwa hali ya kuwa maoni na ushauri au mapendekezo. **Nne**, Kamati zina uhuru wenye mipaka kuhusu utaratibu wake. **Tano**, kazi za Kamati zinaishia kwenye vikao vya Bunge kwa uamuzi wa Bunge. Hii ilionesha kuwa uhuru huo umewekewa mipaka ya kutokukiuka masharti ya Kanuni za Bunge.

Katika toleo lijalo, uhusiano kati ya Bunge na Kamati utafafanuliwa. Ufafanuzi huo utaonesha uhusiano wa kiuwakala na kiuwakilishi. Pamoja na hayo, maelezo zaidi kuhusu umuhimu wa Kamati yatatolewa. Ikumbukwe kuwa yupo mshairi mtajika katika uga wa kibunge, Charles Mloka ambaye aliwahi kuhoji "***Nani mwenye shida ya kuni akaangukiwa na jiti kavu asijitwalie***". Kwa yeyote mpenzi wa masuala ya Bunge, safu hii ni mithili ya jiti kavu kwa wenye shida ya kuni. Kila mfuatiliaji ajiandae kusoma toleo lijalo.

# NMB Bunge Bonanza Lahamasisha Kushiriki Uchaguzi S/Mitaa

*Na Lawrence Raphaely*

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko amewaasa Watanzania wenye sifa kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, 2024 kwa kuchagua viongozi wanaofaa na watakaosaidia kuleta maendeleo nchini.

Naibu Waziri Mkuu ametoa rai hiyo wakati aliposhiriki katika NMB Bunge Bonanza iliyofanyika Agosti 31, 2024 katika viwanja vya John Merlin vilivyopo Jijini Dodoma.

Bonanza hilo ambalo lilihusisha Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge na Wadau mbalimbali kutoka Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali

Aidha michezo ambayo ilishindaniwa wakati wa Bonanza hilo ni pamoja mpira wa miguu, kikapu, wavu, riadha, kuvuta kamba, kukimbiza kuku, kula kwa haraka, kunywa soda na kutembea haraka. Kauli mbiu ya Bonanza hilo ilikuwa ni '**Shiriki uchaguzi kwa Maendeleo ya Taifa"**.

Akizungumza wakati wa Bonanza hilo Naibu Waziri Mkuu alisema Bonanza hilo linapaswa liwe chachu ya kuwakumbusha Watanzania umuhimu wa kuchagua viongozi wanaofaa kwa ajili ya kutuletea maendeleo katika Taifa.

"Bonanza hili litukumbushe kuwa tunaenda kuchagua viongozi wanaofaa kwenye utawala wa nchi hii, Viongozi wa Kitongoji au Mwenyekiti wa Kitongoji au Kijiji hawa ni viongozi muhimu wanaokaa na watu wakati wote tusiwachukulie poa na hivyo wakati wa uchaguzi huu, tuchague viongozi wenye uwezo,'' alisema Dkt. Biteko.

Aliongeza pia kwamba ni muhimu kuzingatia kuchagua viongozi watakaotuunganisha Watanzania kutoka maeneo mbalimbali bila kujali hali zao, dini zao, makabila yao wala vyama vyao vya siasa.

"Uongozi utakaochaguliwa uwe kutokana na sifa na kampeni tusiruhusu kubaguana ama kutukanana badala ya kunadi sera zetu, bonanza hili litukumbushe pia kuwa baada ya uchaguzi maisha yanaendelea na maisha yataendelea tu kama tutachaguana kwa haki, upendo tukisisitiza umoja wa kitaifa na muungano wetu,'' alisema Dkt. Biteko.

Vilevile, Dkt. Biteko aliipongeza Benki ya NMB kwa kuunga mkono juhudi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchangia kiasi cha fedha shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Bunge.

"Nampongeza Spika wa Bunge kwa kufanya ubunifu wa kuwa na Bunge Bonanza ambalo limeleta mageuzi makubwa, kuonesha utu na kufanya Wabunge wafurahie kazi yao na kuruhusu vipaji ili kuwa na Bunge Sports Club pamoja na Bunge Bonanza. Nawapongeza pia waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki michezo mbalimbali katika bonanza hili,'' alisema Dkt. Biteko.

Kwa upande wake, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson aliishukuru Benki ya NMB kwa kuwa wadau wa karibu wa Bunge na Wabunge ambao wamekuwa wakishirikiana kwenye maeneo yao mbalimbali na kuwa bonanza hilo ni sehemu mojawapo.

Alishukuru pia mchango maalum wa NMB ambao walitoa kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Bunge.



*Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akiwaongoza Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Bunge na NMB, na Wadau wengine katika mazoezi ya viungo wakati wa NMB Bunge Bonanza*

"Shule hii inajengwa kwa kuwa Bunge lilishajenga Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bunge na sisi tunatambua kwamba watoto wa kike lazima wapate elimu iliyo bora na watoto wetu wa kiume pia wapate elimu iliyo bora na hivyo tumejenga shule bora ya wasichana na tunajenga ya wavulana na hiyo hii itakuwa imeweka uwiano sawa kuwa Bunge tunathamiani watoto wa kike na wa kiume," alisema Dkt. Tulia.

Pia alitoa wito kwa wadau wengine kuendelea kutoa michango yao ili ujenzi wa shule hiyo ukamilike kwa wakati.

Kwa upande mwingine mwakilishi wa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshmiwa Yahya Rashid Abdulla akizungumza wakati wa Bonanza hilo alisema Baraza la Wawakilishi litaendeleza ushirikiano uliopo kati ya Mabunge hayo mawili.

Naye Mwenyekiti wa Bonanza la Bunge Mheshimiwa Festo Sanga alisema Spika alielekeza Bunge Bonanza lishirikishe wadau wengine na Bonanza hilo limeweza kushirikisha wadau mbalimbali

"Spika alitueleza kwamba ni muhimu kuwa na ushirikiano na taasisi zingine na leo katika bonanza hili tumeshirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Benki ya NMB na wadau wengine kutoka taasisi binafsi," alisema.

Vilevile, Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Bw. Juma Kimori alisema kuwa Bunge limekuwa likishirikiana na NMB kwa masuala ya kifedha na kuwa wanawashukuru wabunge kwa kuendelea kutumia huduma zao pamoja na kushirikiana na benki hiyo katika majimbo yao.

"Katika programu zetu za kurudisha kwa jamii tumekuwa tukishirikiana katika elimu, afya na masuala mbalimbali na NMB



Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko akimpongeza Mheshimiwa Spika kwa Kutwaa Medali wakati wa NMB Bunge Bonanza

itaendelea kushirikiana na ninyi katika kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali," alisema.

Aliongeza kuwa NMB imejikita katika kuleta suluhisho kwa jamii na kwamba kwa sasa wana programu ya kuhakikisha wanafika katika kila kijiji Tanzania ikiwemo programu kama vile mshiko fasta ambapo ni mkopo unaolenga mwananchi wote na hauna masharti kama mikopo mingine.



Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko katika picha ya pamoja na Spika wa Bunge, Mhe. Dkt.Tulia Ackson Viongozi wa Bunge Bonanza pamoja na Viongozi wa NMB, mara baada ya michezo ya Bonanza.

# Watumishi wa Bunge Washiriki Mashindano ya 38 ya SHIMIWI

Na Zanele Chiza

Watumishi wa Bunge la Tanzania wameshiriki mashindano ya 38 ya Shirikisho ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI) yaliyofanyika Mkoa wa Morogoro tarehe 17 Septemba hadi tarehe 06 Oktoba, 2024.

Mashindano ya mwaka huu yalikuwa na Kauli Mbiu inayoeleza "Michezo Huongeza Utendaji Kazi, Shiriki Uchaguzi Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa Endelevu".

Michezo hiyo ilifunguliwa rasmi tarehe 25 Septemba, 2024 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko katika Uwanja wa Jamhuri, Mkoa wa Morogoro.

Akifungua mashindano hayo, Dkt. Biteko alisisitiza Wizara, Taasisi, Mashirika, na Wakala za Serikali kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kushiriki michezo ya SHIMIWI.

Alisema mashindano ya SHIMIWI yanafanyika kwa mujibu wa sheria hivyo fedha zake zitengwe kila mwaka na kama kuna changamoto zibainike na kufanyiwa marekebisho

"Kama tumekubaliana kufanya jambo, lazima tulifanye jambo kuwa la lazima na siyo hiari, kama kuna sababu ya kuliboresha, tuboreshe na kufanya mabadiliko.

Agizo hilo alilitoa baada ya kushuka kwa idadi ya vilabu vinavyoshiriki mashindano hayo kutoka 74 mwaka 2023 hadi 66 mwaka 2024.

Alisema hali hiyo inaonesha ipo changamoto na hivyo kuwaagiza waajiri ambao hawakutuma washiriki kutoa maelezo juu ya uamuzi wao kwaajili ya hatua za siku zijazo.

Aidha, aliwasisitiza watumishi wote wa umma kujiandikisha na kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, 2024 ili waweze kuchagua viongozi bora kwa ajili ya Taifa la Tanzania.

"Najua mnaendelea na SHIMIWI kwa siku kadhaa, viongozi waangalie namna ya kuwapa fursa ili mjiandikishe kwa ajili ya kuwachagua viongozi wenu" Alisema Mhe. Dkt. Biteko.

Mheshimiwa Dkt. Biteko pia aliwataka watumishi wa umma kuendelea kutoa huduma kwa Watanzania bila kuzingatia tofauti zao, kuzingatia matumizi bora ya TEHAMA, ushirikishwaji wa Serikali na Sekta Binafsi katika kuleta maendeleo ya pamoja na kushirikisha makundi ya watu wenye mahitaji maalum.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora, Juma Mkomi aliwataka watumishi wanaoshiriki mashindano hayo, mbali na kutumia michezo kuboresha afya, vilevile watumie michezo hiyo kujenga mtandao wa kufahamiana na kuelimishana katika masuala ya kazi.

Awali, Mwenyekiti wa SHIMIWI, Daniel Mwalusamba alisema lengo la michezo hiyo ni kuwajenga watumishi kuzingatia misingi ya uzalendo, kujitolea kulipa kodi, kuwa wasikivu kwa Serikali iliyopo madarakani.

Hata hivyo alisema michezo inakabiliwa na changamoto ikiwemo kushuka kwa mahudhurio kwa idadi ya vilabu nchini.

Timu ya Bunge ilianza michuano ya mwanzo vizuri na kuweka rekodi ya kufunga magoli mengi zaidi katika mchezo wa Mpira wa pete baada ya kuifunga timu ya Pamba magoli 75 kwa moja.

Hata hivyo timu hiyo ilitolewa hatua ya robo fainali kwa mchuano mkali ambapo Bunge ilipata magoli 43 na Timu ya Hazina ilipata magoli 44.

Mchezo wa kuvuta kamba wanaume, Mchezo wa Bao, riadha, darts ziliweza kuingia robo fainali ambayo ni 16 bora za michezo ya SHIMIWI.

Kwa upande wa mchezo wa *darts* na riadha Bunge walifika hatua ya fainali huku kwenye mbio za wazee Bunge waliweza kupata medali ya ushindi wa pili.




*Timu ya Watumishi wa Ofisi ya Bunge ya mpira wa pete katika picha ya pamoja, wakati wa mashindano ya 38 ya SHIMIWI,Mkoani Morogoro*

Michezo inayofanyika katika mashindano hayo ni mpira wa miguu, mpira wa pete, kuvuta kamba, karata, bao pamoja na michezo ya jadi.

Watumishi wa Umma kutoka Ofisi mbalimbali hushiriki katika mashindano hayo na kupata vikombe siku ya mwisho ya kufunga mashindano hayo.



*Timu ya Watumishi wa Ofisi ya Bunge ya Kuvuta kamba ya Wanawake katika mashindano ya 38 ya SHIMIWI, yaliyofanyika Mkoani Morogoro*



*Timu ya Watumishi wa Ofisi ya Bunge ya Mpira wa Miguu katika mashindano ya 38 ya SHIMIWI, yaliyofanyika Mkoani Morogoro*




Limeandaliwa na:
Ofisi ya Bunge, Mtaa wa Makole
S.L.P 941
41105 DODOMA
Nukushi: +255 26 2324218 Simu: +255 26 2322761-5
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz



bunge-tz
bunge.tanzania
Bunge la Tanzania
Bunge TV
www.bunge.go.tz